





**Mbaroni** kwa madai kuua mtoto na kumtupa mtoni UKURASA 5





# Nipashe

Jumatano Aprili 13, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580914

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


## RIPOTI YA CAG

# NI KUFURU

• **NHIF** yalipa mamilioni wanaume 730 kujifungua, utata wanachama 444 kupimwa damu siku moja...

*Endelea ukurasa 2*



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), Charles Kichere, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, wakati akitoa ufafanuzi kuhusu ripoti ya ukaguzi wa hesabu za serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, mwaka 2020/2021. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Sekta kipaumbele ajira mpya 32,600 serikalini zabainishwa

UKURASA 3

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**VYOO SAFI NA SALAMA NCHINI SASA NI 73%**

SUALA la mabadiliko ya tabia na mitazamo bora juu ya utunzaji wa mazingira limepewa...

UKURASA WA 4

**MPANGO: TAASISI ZISIZOTOA GAWIO ZIANZE KUJITATHMINI**

WAKATI Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Airtel Tanzania PLC ikiikabidhi serikali...

UKURASA WA 4

**SITA WALIVYOFARIKI WAKIENDA MSIBANI**

WATU sita wamefariki dunia na wengine 19 kujeruhiwa baada ya Costa yenye namba za...


## Balozi Marekani, Mbowe wahimiza demokrasia kwa maendeleo ya nchi

UKURASA 3


**MICHEZO** SIMBA YATAKA KUVUNJA REKODI CAF UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## RIPOTI YA CAG

# NI KUFURU

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2020/21 imewasilishwa bungeni, ikiibua dosari kadhaa ikiwamo kufuru ya wanaume 731 kugharimu mamilioni ya shilingi Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa madai ya kupata huduma za upasuaji na kujifungua.

Rais Samia Suluhu Hassan kupitia wasaidizi wake, jana alitimiza matakwa ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Tanzania kwa kuiwasilisha taarifa hiyo ya CAG bungeni jijini Dodoma ikiwa na ripoti 20.

Kwa mujibu wa CAG Kichere, ripoti hizo ni za: Serikali Kuu; Mamlaka za Serikali za Mitaa; Mashirika ya Umma; miradi ya maendeleo; ukaguzi wa ufanisi; ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA; ukaguzi maalum wa mifumo ya TEHAMA inayohusu mapato; na ya ufuatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti za ukaguzi wa ufanisi wa miaka iliyopita.

Pia, zimo ripoti za ukaguzi wa ufanisi 12 zinazohusu: Usimamizi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo; ukarabati wa barabara unaotekelezwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS); uendelezaji na utangazaji wa utalii; upangaji na utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Vile vile, usimamizi wa Makumbusho ya Taifa; utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kwenye Sekta ya Madini; usimamizi na utoaji wa huduma kwa mahabusu; usimamizi wa usajili wa biashara na utoaji wa leseni; usimamizi wa mifumo ya ardhioevu; mfumo wa haki-jinai Tanzania; utoaji wa fedha na usimamizi wa mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na utekelezaji wa shughuli za udhibiti wa vipimo.

**KUFURU NHIF**

Katika ripoti yake kuhusu ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA, CAG Kichere alisema amebaini mfumo wa AMMIS unaotumiwa na NHIF, ulikuwa na wafanyakazi 2,495 wa sekta binafsi kutoka kampuni 87 waliosajiliwa katika kundi la wafanyakazi wa umma.

Vilevile, alisema kuwa alibaini wachangiaji 165 wanaochangia kwenye mfuko wenye wategemezi zaidi ya watano, wategemezi 73 waliosajiliwa kama wanachama, na kuwapo kwa wanufaika 731 wa kiume wenye taarifa zinazoonyesha kuwa walipata huduma ya upasuaji (C/S) au huduma za kawaida za kujifungua.

"Nilihakiki na kubaini madai batili yaliyowasilishwa na vituo vya afya kwenda NHIF na kulipwa Sh. 14,409,200. Nilibaini kuwapo kwa madai 56 yanayoonyesha wanaume waliopata huduma ya upasuaji (C/S) au huduma za kawaida za kujifungua.

"Pia, nilibaini kuwapo kwa wanachama 444 waliopata huduma ya kuchunguzwa picha kamili ya damu (full blood picture) zaidi ya mara moja kwa siku moja kwenye kituo kimoja (yaani hadi mara 30)," alisema.

**MIWANI MARA MBILI**

CAG pia alisema alibaini kuwapo kwa malipo ya madai yanayorudiwa pamoja na madai yanayoonyesha wanachama wa NHIF waliopokea miwani ya kusomea zaidi ya mara moja wakati utaratibu unaruhusu kutoa mara moja kwa mwaka.

**MALIPO WASIOSTAHIKI**

CAG alisema Kifungu cha 27(2) cha Sheria ya Taifa ya Bima ya Afya ya mwaka 2019 kinaeleza kuwa mfuko unaweza kukataa au kupunguza malipo ya madai ambayo ni ya uongo au yasiyo sahihi au pale mdai anaposhindwa bila sababu za msingi kuzingatia sheria au kanuni zinazohusu malipo ya madai yaliyotolewa chini ya sheria hiyo.

Alisema kuwa alihakiki madai yaliyolipwa kwa kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Juni 2021 na kubaini kuwapo kwa madai 7,556 yaliyolipwa yenye jumla ya Sh. 69,175,190 ambayo yana majina yasiyo sahihi ya wapokeaji huduma kulinganishwa na majina ya wenye kadi kwa namba za kadi husika.

CAG alisema udhaifu huo umesababishwa na udhibiti duni katika kuhakiki majina ya wenye kadi wakati wa kushughulikia madai.

"Ni maoni yangu kuwa malipo ya madai yamesababisha hasara isiyopungua Sh. 69,175,190 na kutengeneza mwanya wa kulipa madai ya huduma zinazotolewa kwa watu wasiostahiki.

Alisema anapendekeza serikali kuboresha mfumo wa CMIS ili kuhakikisha kuwa unaidhinisha majina ya wapokeaji huduma dhidi ya majina ya wenye kadi wakati wa uchakataji wa madai.

**HASARA HOSPITALINI AMANA**

Alilinganisha huduma zinazotolewa kwa wanachama wa NHIF na Hospitali ya Rufani Amana yenye kanzi-data ya wanachama wa NHIF na kubaini wagonjwa 325 katika e-HMS ambao walipewa huduma kama wanachama halali wa NHIF ilhali hawakuwa wanachama.

Alisema hitilafu hiyo ilisababishwa na udhaifu katika ushirikiano kati ya mfumo wa e-HMS na NHIF na hasara iliyoipata Hospitali ya Amana kutokana na dosari hiyo haitarejeshwa na NHIF.

**HASARA YAPUNGUA ATCL**

Akizungumzia mashirika ya kibiashara yaliyopata hasara kwa miaka miwili mfululizo (2019/20 na 2020/21), CAG Kichere alisema mashirika 14 yalipata hasara mfululizo na hali hiyo ilisababishwa na hasara kwenye uwekezaji uliofanywa, ufanisi duni wa mashirika husika na udhibiti hafifu wa mapato na matumizi.

Hata hivyo, licha ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kuwa miongoni mwa mashirika hayo, CAG alisema mwenendo wa kampuni hiyo unaonyesha kuimarika kulinganisha na mwaka uliopita kwa kuwa mwaka 2020/21 kampuni iliongeza mapato kwa asilimia 11 na kupunguza matumizi kwa asilimia tatu.

"Kampuni ilipunguza hasara ya jumla kutoka Sh. bilioni 60.25 mwaka 2019/20 hadi kufikia Sh. bilioni 36.18 mwaka 2020/21. Napendekeza kwamba kampuni zinazopata hasara, ziimarishe ufanisi katika utendaji na kuchukua hatua madhubuti kupunguza gharama zisizo na ulazima," alisema.

**UFUJAJI BANDARI**

CAG alisema kuwa kwa kipindi cha miaka mitano na miezi mitatu kuanzia Januari Mosi 2015 mpaka Machi 31, 2020, jumla ya hundi 7,888 zilitumika kutoa fedha Sh. bilioni 31.76 kutoka akaunti ya benki ya matumizi ya Bandari ya Mwanza.

Kati yake, hundi 4,777 za Sh. bilioni 18.41 ziliwasilishwa na Benki ya CRDB tarehe 30 Novemba 2020 kwa ajili ya ukaguzi. Kati yake, hundi 2,043 za Sh. bilioni 8.38 zilitumika kutoa fedha taslimu bila kuandaliwa vocha za malipo na ushahidi wa nyaraka za matumizi.

## Mkandarasi alipwa bil. 19.5/- kisa kukatika umeme Bwawa la Nyerere

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini suala la mkandarasi wa mradi wa kufua umeme wa Bwawa la Mwalimu Nyerere kulipwa Sh. bilioni 19.5 kutokana na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Akitoa mukhtasari wa ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa jana, CAG Charles Kichere, alisema kukatika kwa umeme kwenye mradi kumesababisha madai ya dola za Marekani milioni 8.53.

CAG alifafanua kuwa alibaini tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara kwenye eneo la mradi kuanzia tarehe 10 Januari 2020 hadi Oktoba 2020 na hakuna tathmini ya kina iliyofanywa kuainisha mahitaji ya umeme wa kuendesha vifaa vya mkandarasi kwenye eneo la mradi.

"Kukatika kwa umeme mara kwa mara kumesababisha mkandarasi kudai dola za Marekani milioni 8.53 (sawa na Sh. bilioni 19.51).

"Hii ilisababishwa na kukosa tathmini inayoainisha mahitaji ya umeme wa kuendesha vifaa vya mkandarasi kwenye eneo la mradi. Kukatika kwa umeme kwenye eneo la mradi kunaongeza muda na gharama za kukamilisha mradi.

"Ninapendekeza menejimenti ya TANESCO ifanye tathmini ya kina ya mahitaji ya umeme wa kuendesha vifaa na mitambo kwenye eneo la mradi ili kupata takwimu halisi za nishati inayohitajika," alisema.

Pia alisema hadi kufikia Oktoba 31, 2021, mradi ulipangwa kukamilika kwa asilimia 94.47 lakini alibaini ulikamilika kwa asilimia 48.02, ukiwa umechelewa kwa asilimia 46.45.

Alisema ucheleweshaji umesababishwa na kuchelewa kuwasilishwa na kuidhinishwa kwa usanifu wa mwisho wa mradi, janga la mafuriko kwenye Mto Rufiji pamoja na janga la UVIKO-19.

"Ninapendekeza kwamba, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) liwasiliane na mkandarasi ili kuandaa mpango mkakati utakaoainisha mbinu zitakazotumika kuharakisha utekelezaji wa kazi za mradi ili kufidia muda uliopotea.

"Aidha, shirika lifanye tathmini ya gharama za ziada na madhara ya kimkakati yanayotokana na kuchelewa kwa mradi na kuwezesha serikali kuchukua hatua madhubuti," alisema.

**POS ZACHEZEWA**

CAG pia alisema kuwa katika kipindi cha miaka ya fedha 2019/20 na 2020/21 katika Halmashauri ya Ilala, alibaini mawakala wawili walikusanya kwa kutumia mashine za POS Sh. milioni 131.07 na Sh. 289,500 mtawalia.

Hata hivyo, mawakala hao walirejesha nyuma muda katika mashine za POS kwa kuonyesha makusanyo hayo yalifanyika kati ya mwaka 2008 na 2017, kipindi ambacho hata namba za utambulisho zilizotumika hazikuwa zimesajiliwa katika mfumo wa makusanyo ya mapato.

"Hii ilisababisha makusanyo kutotambulika na kuwasilishwa benki katika miaka husika. Ninapendekeza serikali ichukue hatua stahiki kwa watumishi na mawakala waliosababisha hasara hiyo," alisema.

**UHABA WA WALIMU**

CAG pia alisema tathmini ya uwiano wa walimu na wanafunzi katika mamlaka 48 za serikali za mitaa ilibaini kuwa kati ya walimu 40,458 wanaohitajika kwa shule za msingi, walikuwapo walimu 23,881 tu ikimaanisha upungufu wa walimu 16,571, sawa na asilimia 41.

"Hali hii inadidimiza juhudi za serikali katika kuboresha elimu ya msingi na sekondari. Ninapendekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutathmini changamoto nilizozibaini ili kuboresha elimu ya msingi na sekondari," CAG alisema.

Ujamaa Community Resource Team
EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP

**TERMS OF REFERENCE**
**Development of gender-based sensitive LUP Approach**

**Location: Arusha**
**Application Deadline: 26-April 2022 (5 pm)**
**Languages Required: English**
**Starting Date: 28th April 2022**
**(Date when the selected candidate is expected to start) 28th April 2022**
**Duration of Initial Contract: two months**

Ujamaa-Community Resource Team (UCRT) is a non-profit environmental and social justice organization, which works with indigenous groups of different cultures. The target communities are those who depend on communal resource management regimes to support their livelihood.

Specific tasks and scope of the consultancy the scope of the assignment will include the following:

- Literature review of relevant Land and natural resources, Land laws, Policies, strategies,
- Propose an appropriate approach that will enhance gender equity, learning, and application of skills in gender mainstreaming in the land use plan process.
- Prepare a Compact of normative gender equality and women's empowerment commitments, drawing from national land and natural resource laws and policies.
- Organize meetings and Interviews with UCRT staff to observe the existing gender mainstreaming approaches and meet other external stakeholders for diverse knowledge.
- Recommendation that leads to the development of gender-based sensitive LUP Approach

**Qualifications and Experience**

- Advanced University Degree (Masters or equivalent) in Gender Studies, Social Sciences, Human Rights, Development Studies, or related field.
- At least ten (10) years of relevant professional experience in designing and delivering gender mainstreaming training including gender budgeting) in the Public Sector, International or Regional Organization.
- Demonstrated experience in curriculum or training materials development for adult learners, especially in the area of gender training.
- Good knowledge of gender perspectives in all pillars of gender equality
- Excellent facilitation, presentation, and writing skills
- Fluent in spoken and written English and Swahili.

**Language Requirements:**
Fluent in written and spoken Swahili and English.

**Submission**
Interested candidates are requested to submit an electronic copy of their expression of interest/proposal to **manager@ujamaa-crt.or.tz** not later than **April 26th, 2022**

216803302




Mkurugenzi Mtendaji Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Ndomba, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa tuzo ya mwajiri bora wa mwaka 2022 huku akionyesha kitabu cha mwongozo kwa wanachama, washiriki, watakaotaka kushiriki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Sekta kipaumbele ajira mpya 32,600 serikalini zabainishwa

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

SERIKALI imezitaja sekta za kipaumbele katika ajira kwa watumishi wapya 32,604 huku ikibainisha kwamba inatarajia kutumia Sh. bilioni 49.4 kwa mwezi kutokana na ajira hizo pamoja na kupandisha madaraja watumishi 125,223.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuelezea utekelezaji wa ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusiana na ajira mpya na usimamizi wa stahiki za watumishi wa umma.

Mhagama alisema jkwa mujiubu wa vipaumbele vya kisekta, elimu imetengewa nafasi za ajira 12,035, afya 10,285, kilimo 814, mifugo 700, uvuvi 204, maji 261 na sheria 513.

Kutokana na ajira na upandishaji huo madaraja, alisema Sh. 26,297,541,175 zitatumika kuajiri watumishi wapya 32,604 na Sh. 23,078,224,169.50 zitatumika kuwapandisha madaraja watumishi 92,619.

Kuhusu ajira mpya kwa watumishi wa umma, Mhagama alisema mchakato utasimamiwa na utasimamiwa na wizara husika za kisemta kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Alisema licha ya kuajiri na kuwapandisha madaraja watumishi hao, serikali pia itatumia Sh. 824,441,522.00 kuwabadilisha vyeo na kada watumishi 6,026 waliotengewa ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2021/22 kuanzia Mei Mosi, mwaka huu.

"Uamuzi huu wa serikali wa kuwapandisha vyeo na kuwabadilisha kada watumishi wa umma, utaongeza ari, motisha na uwajibikaji wa hiari kwa watumishi wa umma katika kutoa huduma bora kwa wananchi," alisisitiza.

Waziri alisema ni wakati muafaka kwa watumishi wa umma kuenzi juhudi za Rais Samia za kuboresha masilahi ya watumishi wa wmma kwa kufanya kazi kwa bidii, weledi na bila kushurutishwa katika kuwahudumia wananchi.

Kuhusu kusogeza huduma karibu na wananchi hususan maeneo ya pembezoni, Mhagama alizielekeza mamlaka za ajira kutoa kipaumbele cha ajira kwenye maeneo hayo ili wananchi wanufaike na huduma zinazotolewa na serikali kupitia taasisi zake.

Katika kuhakikisha haki inatendeka katika fursa hizo za ajira, Mhagama aliziagiza mamlaka za ajira katika utumishi wa umma kuendesha michakato ya ajira kwa uwazi, weledi, uadilifu na kutoa fursa sawa kwa waombaji wote kushiriki katika mchakato na hatimaye serikali kupata watumishi mahiri na wenye sifa stahiki.

Aidha, aliwataka waajiri wote nchini kuhakikisha watumishi wa umma wapya wote watakaoajiriwa wanapata mafunzo elekezi kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma kabla ya kupangiwa vituo vya kazi kama ilivyoelekezwa na serikali, kuwapangia majukumu stahiki watumishi hao na kusimamia ipasavyo rasilimaliwatu iliyopo kwenye maeneo yao ya kazi ili kuleta tija kwa maendeleo ya taifa.

# Balozi Marekani na Mbowe wasisitiza demokrasia bora

**Na Christina Mwakangale**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amekutana na Balozi wa Marekani, Donald Wright, na kufanya mazungumzo, huku akisisitiza umuhimu wa upinzani kwa demokrasia yenye afya inayoruhusu maoni ya wengi.

Katika ukurasa wa twita, Balozi Wright alisema: "Ni hatua kubwa kukutana na Freeman Mbowe. Upinzani mahiri wa kisiasa ni muhimu kwa demokrasia yenye afya na demokrasia yenye afya inaruhusu maoni mengi tofauti.

"Nitaendelea kufanya kazi na wadau wote kupanua wigo wa ushiriki wa kisiasa."

Mwishoni mwa wiki, Mbowe alisema moto wa siasa umewashwa ndani ya chama hicho huku akiahidi kufanya kazi usiku na mchana kuwafikia Watanzania.

Kiongozi huyo alitoa kauli hiyo wakati wa ziara yake jimbo la Kawe, ikiwa ni kampeni ya mguu kwa mguu kuzungumza ana kwa ana na wananchi pamoja na kukusanya fedha za kujenga chama.

Mbowe alisema ziara hiyo ni mwendelezo wa oparesheni ya 'Join the Chain' yenye lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya ujenzi wa chama hicho pamoja na kutoa elimu ya uraia kwa wananchi.

Akizungumza na wananchi wa Tegeta na kata ya Kunduchi, Mbowe alisema matembezi hayo yatakuwa kwa miguu ndani ya mitaa ya Dar es Salaam na kwamba pamoja na mambo mengine ni kuwashukuru Watanzania kwa kupigania uhuru wake alipokuwa gerezani.

"Ninatembea kama mnavyoniona kuwasalimia wananchi, nikitambua namna mamilioni ya Watanzania walivyolilia uhuru wangu na vijana wangu nilipokuwa gerezani. Kwa hiyo napita kuwasalimia kuwashukuru namna ambavyo mlitetea haki yetu na uhuru wetu. Asanteni sana na Mungu awabariki," alisema.

Mbowe aliongeza kuwa kazi ya siasa haijafika mwisho bali imechochewa moto kwa kuwa chama hicho kitatembea usiku na mchana kuhakikisha kuwa wanaliamsha taifa ili litambue namna ya kutetea watu wake.

"Tutatembea usiku na mchana kwa jasho na damu kuhakikisha tunaliamsha taifa hili lijitambue, lijue namna ya kutetea haki na uhuru wa nchi yake, namna ya kuibana serikali yetu itambue kwamba maisha ya wananchi yamekuwa magumu, waache kuongeza tozo, ili maisha ya wananchi yawe nafuu," alifafanua.

Kwa mujibu wa Mbowe, wajibu wa kulitetea taifa ni wa kisiasa na kuwataka wananchi wa Tegeta kumuunga mkono katika wajibu huo ili kupaza sauti kwa pamoja.

"Lazima tupaze sauti zetu. Hatuwezi kuendelea kuwa taifa la kuoneana, kudhulumiana, la kunyanyasana na taifa la ubaguzi wa kiitikadi. Asanteni Kawe kwa mapokezi mazuri, Tegeta nitaendelea kuwa na ninyi, hakuna kulala mpaka kieleweke," alisema.

Baada ya kuzungumza, Mbowe alianza kukusanya michango ya hiari kutoka kwa wananchi hao kwa ajili ya kusaidia kujenga chama huku akisisitiza kuwa kitajengwa na wananchi wenye uwezo mdogo ambao hutoa fedha zao kama sadaka ya ukombozi na si matajiri pekee.

**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LTD**

TANESCO

**Tender No. PA/001/2021-2022/HQ/G/177**

**For**

**PRE QUALIFICATION OF SUPPLIERS OF DISTRIBUTION MATERIALS UNDER TWO YEARS FRAMEWORK AGREEMENT**

**NOTICE TO THE PUBLIC**

**Date: 13/04/2022**

**TANESCO** hereby informs the public that, the above mentioned Tender has been uploaded to **TANePS on 11.04.2022.** Interested applicants can access the Pre –Qualification Document through **www.taneps.go.tz**

**MANAGING DIRECTOR**
**TANESCO LIMITED**

# Mpango: Taasisi zisizotoa gawio zijitathmini

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKATI Kampuni ya Mawasiliano ya Simu ya Airtel Tanzania PLC ikiikabidhi serikali Sh. bilioni 143 kama gawio, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango amezitaka taasisi binafsi ambazo serikali imewekeza hisa hata kama ni asilimia moja, kujiendesha kwa ufanisi na kulipa gawio.

Pia amezitaka taasisi zisizotoa gawio kujitathmini kwa kuwa serikali iliwekeza ili faida itumike kwa maendeleo ya wananchi. Dk. Mpango alitoa maagizo hayo wakati akipokea hundi ya Sh bilioni 143 iliyotolewa na Airtel kwa mwaka wa fedha 2021/22 ikiwa ni gawio, mchango wa uwezeshaji na mauzo ya minara. Airtel Tanzania inamiliki asilimia 51 ya hisa zote wakati serikali ni mmiliki kwa asilimia 49.

"Taasisi ambazo bado zinatoa gawio dogo na zile ambazo bado zinajiendesha kwa faida, lakini hazitoi gawio stahiki zinatakiwa kujitathmini na kuhakikisha zinafanya vizuri na kulipa gawio serikalini," alisema Dk Mpango.

Kampuni hiyo kubwa ya pili kwa umiliki wa soko la mawasiliano ya simu nchini, imesema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 88 ni gawio, Sh. bilioni 12 mchango wa uwezeshaji (Support Services Agreement - SSA) na Sh. bilioni 43 ni kutokana na mauzo ya minara ya mawasiliano ya Airtel kwenda kwa Minara Tanzania Limited.

Akikabidhi hundi hiyo ya mfano kwa Makamu wa Rais, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Airtel Tanzania PLC , Gabriel Malata, alisema Sh. bilioni 88 ambazo serikali imelipwa zimeweka rekodi ya kuwa kiasi cha juu kulipwa kama gawio kwa kampuni ambazo serikali inamiliki hisa.

"Tunapongeza juhudi za serikali za kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa mfumo wa ubia, ambapo leo hii tunashuhudia mafanikio mazuri ya Airtel Tanzania " alisema Malata.

Alisema kwa miaka mitatu sasa, Airtel Tanzania PLC imeilipa serikali ya Tanzania zaidi ya Sh. bilioni 200 zinazotokana na gawio, mchango wa uwezeshaji wa huduma na malipo mbalimbali. Pia alisema kampuni imelipa ada na tozo zilizowekwa kwa mujibu wa sheria ambazo ni Sh. bilioni 97 kwa mwaka wa fedha 2020/21.

Aidha, Malata alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio chanya ya kampuni hiyo kufikia kuilipa serikalini gawio la Sh. bilioni 143.

"Airtel tunaamini kwamba kutokana na serikali kuweka mazingira bora ya uwekezaji, wawekezaji wazawa na wale wa kutoka nje wataendelea kushirikiana na serikali kama ilivyo kwa Airtel sasa." alisema Malata.Pia alitoa shukrani kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Ofisi ya Msajili wa Hazina, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Tume ya Ushindani (FCC), Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa mafanikio yote.

Makamu wa Rais, Dk Mpango ambaye alimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan alisema serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri na endelevu ya kufanya biashara.

Aidha, Dk. Mpango alimpongeza Msajili wa Hazina kwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa makubaliano yanayowezesha kupatikana kwa fedha na Airtel kuendelea kulipa shilingi bilioni moja kila mwezi.

"Tukio hili la leo linaashiria uwepo wa mazingira mazuri ya kiutendaji na mahusiano thabiti ya kibiashara baina ya wabia. Mapato haya yalipatikana yana faida kubwa sana katika kuchangia miradi mikubwa ya maendeleo nchini na kuboresha huduma za jamii ikiwemo afya, elimu na maji kwa Watanzania wote. Niwasihi tena tuendeleze jitihada hizi ambazo ndiyo chachu ya maendeleo ya nchi yetu na manufaa kwa kila mwananchi." alisema Dk. Mpango.

Hata hivyo, alitaka kampuni hiyo kujiimarisha na kuendelea kutoa mchango wake kwa manufaa ya taifa na wananchi.

Naye Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto, akizungumza katika hafla hiyo alisema mikataba iliyotiwa sainiwa baina ya serikali na Bharti Airtel ambayo ilikuwa na mambo makubwa na yenye tija kwa wabia wote na wananchi kwa ujumla wamesimamia vyema na matokeo yanajidhihirisha katika ufanisi wa mapato na michango isiyo ya kodi ambayo wameitoa.

Aidha, alisema Ofisi ya Msajili wa Hazina imeendelea kupata mafanikio katika ukusanyaji wa fedha za serikali.




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (wa tatu kushoto), akipokea mfano wa hundi ya Sh. Bilioni 143 ikiwa ni gawio, mchango wa uwezeshaji na mauzo ya minara kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Simu ya Airtel, Gabriel Malata (wa pili kushoto) pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh (kushoto), jijini Dodoma jana. Wengine Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (wa pili kulia), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande (wa tatu kulia) na Msajili wa Hazina, Mgonya Benedicto. **PICHA: OMR**

# Mradi wawezesha uwapo vyoo safi, salama kwa 73%

**Na Mary Kadoke**

SUALA la mabadiliko ya tabia na mitazamo bora juu ya utunzaji wa mazingira limepewa kipaumbele ili kutokomeza maradhi yanayoambukizwa kwa njia ya maji yanayoigharimu serikali Sh. bilioni 460 kila mwaka kwa ajili ya tiba.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitoa kauli hiyo juzi mkoani Dar es Salaam katika maadhimisho ya miaka mitano ya mradi wa 'Usichukulie poa nyumba ni choo,' uliofanikisha uwapo wa vyoo safi na salama nchini kwa asilimia 73.

Alisema licha ya serikali kujikita kupambana kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu juu ya usafi wa mazingira, tabia na mitazamo mibaya ya watu juu ya utunzaji wa mazingira imekuwa ikikwamisha juhudi za kutimiza malengo hayo.

"Usafi hasa usafi wa vyoo ni suala linalopewa kipaumbele duniani na nchini kwa ujumla; lengo lilkiwa kuhakikisha kila nyumba na kila mahali panakuwa na choo kisafi kufikia mwaka 2030," alisema Ummy.

Akinukuu ripoti ya Benki ya Dunia, alisema wagonjwa wanane hadi kumi wa nje (OPD) wana matatizo ya kiafya yatokanayo na uchafu wa mazingira.

Aidha aliongeza kuwa ripoti hiyo ilieleza kuwa watu hutumia saa 58 kwa mwaka kutafuta maeneo yasiyo halali kujihifadhi (kupata haja ndogo au kubwa).

Balozi wa Uingereza nchini, David Concar, alipongeza ushiriki wao katika kampeni hiyo, na jinsi kampeni hiyo ilivyochagiza harakati za Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, juu ya mazingira katika kampeni yake ya 'Mtu ni Afya' ya mwaka 1971.

Alisema mikakati hiyo imesaidia kukuza ajenda ya usafi wa mazingira yaliyoshawishi watu kuthamini na kubadilisha mitazamo mibovu inayogusa mazingira.

Mratibu Mkuu wa kampeni hiyo kutoka taasisi ya Project Clear, Kaposo Mwambuli, alipongeza serikali na wadau wote waliosapoti kampeni hiyo tangu awali, na kuwa jitihada hizo zimezaa matunda na kuifanya Wilaya ya Njombe iliyokuwa na miundombinu mibovu ya vyoo kufikia asilimia 100 ya lengo la mradi.

"Nichukue fursa hii kumshukuru aliyekuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, aliyezindua mradi huu mwaka 2018 jijini Dodoma. Kwa upande mwingine shukurani ziende kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuwahimiza makatibu tawala wa mikoa kutekeleza mradi huo kikamilifu."

## Sita walivyofariki wakienda msibani

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

WATU sita wamefariki dunia na wengine 19 kujeruhiwa baada ya Costa yenye namba za usajili T 833 DMH, lililokuwa kwenye mwendo kasi kugonga nguzo na kutumbukia darajani kutokana na dereva kushindwa kulidhibiti.

Akizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (Magunga), Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Safia Jongo, alithibitisha ajali hiyo kutokea saa tisa alfajiri kuamkia jana wakati gari hilo likitokea Dar es Salaam kuelekea mkoani Kilimanjaro kupeleka msiba.

Jongo alisema vifo vilivyotokana na ajali hiyo ni vya wanawake watatu na wanaume watatu na ilitokea katika eneo la Kwamduru, Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga, kati ya wanawake hao mmoja alikuwa ni mtoto mwenye umri kati ya miaka miwili na minne na miili mitano imeshatambuliwa na ndugu zao, huku mmoja ukiwa haujatambuliwa na hali za majeruhi zinaendelea vizuri katika Hospitali ya Magunga.

"Costa ni zile zinazokodishwa, inavyoonekana alitengeneza mazingira kama wamekodiwa, walipopita sehemu mbili askari waliwakagua, walikuwa na vibali vyote na walikuwa wanaelekea msibani Kilimanjaro," alisema Kamanda.

"Kwasababu wakitoka huko huwa wanakubaliana waseme wamekodiwa, lakini baada ya ajali hii kutokea kufanya mahojiano ya kina na abiria, walisema kwamba pale Ubungo walikatiwa tiketi na kuingia kwenye gari kama abiria," alibainisha.

"Natoa wito kwa wananchi, kutokana na ajali hii tujifunze, vitu vyote ambavyo huwa havifuati taratibu, basi mwisho wake sio mzuri, safari za usiku ambazo sio rasmi matokeo yake yanakuwa kama haya," alisisitiza.

Pia, Kamanda Jongo alisema dereva wa gari hilo ni miongoni mwa majeruhi na amelazwa hospitalini hapo akipatiwa matibabu chini ya ulinzi wa jeshi la polisi, na kuongeza kuwa mara kwa mara wanatoa maelekezo kwa madereva kuwa makini kwa kutoendesha mwendo wa kasi na kuheshimu sheria na alama za barabarani.

"Niendelee kuwasihi madereva wafuate sheria na alama za barabarani wasisubiri mpaka wakutane na askari, hii itatusaidia kupunguza hivi vifo, kila mwananchi awe ni balozi wa usalama barabarani, pale anapoona dereva anaendesha mwendo hatarishi atoe taarifa kwa sababu majeruhi hawa wanakiri kwamba pale ambapo dereva wao alipokaribia kuwafikia polisi alikuwa akiendesha mwendo wa taratibu," alisema.

Naye Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Korogwe, Dk. Salma Swed, akiongea kwa njia ya simu, alikiri kupokea miili ya marehemu na majeruhi alfajiri ya kuamkia Jumanne.

Alisema wamepokea miili ya marehemu sita na majeruhi 19, wawili kati yao hali zao ni mbaya na wamewahamishia katika Hospitali ya Rufani Bombo.

masuala mbalimbali yanayohusu ukusanyaji kodi. **PICHA: TRA**



## Waajiri bora kupewa tuzo

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha Waajiri Tanzania (ATE) kimeandaa tuzo ya mwajiri bora wa mwaka 2022 ambayo itawatambua waajiri wenye misingi bora ya usimamizi wa nguvu kazi na rasilimali watu.

Mkurugenzi Mtendaji na Ofisa Mtendaji Mkuu wa ATE, Suzanne Ndomba-Doran, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam na kufafanua kuwa tuzo hizo pia zitatambua waajiri wanaofanya biashara kwa kuzingatia sheria na taratibu.

Alisema marejeo ya uboreshaji wa mchakato wa tuzo hizo uliofanyika kwa kushirikana na mshauri mwelekezi umesababisha kwa mwaka huu ziwe na vipengele 14 kutoka 27 vya awali.

"Vipengele vinne vipya ni pamoja na namna ambavyo kampuni zinakabiliana na majanga yanayotokea katika maeneo yao ya kazi mfano janga la UVIKO-19, mabadiliko ya tabianchi.

Alitaja vingine ni haki na usawa wa kijinsia na kingine ni ukidhi wa matakwa ya kisheria.

Alisema lengo la kufanya mabadiliko hayo ni kuendelea kuziboresha tuzo hizo na kuongeza ushindani miongoni mwa washiriki.

Pia, alisema ni kujaribu kugusa kila eneo ambalo litaleta tija katika ukuzaji na uendelezaji wa biashara na rasilimali watu katika eneo la kazi.

Kiongozi huyo alisema tangu kuanzishwa kwa tuzo hizo mwaka 2005, zimeendelea kuhamasisha waajiri kuendelea kurekebisha na kufanya vizuri zaidi katika maeneo mbalimbali mahala pa kazi pamoja na kuzingatia sheria na kanuni.

"Miaka miwili mfululizo (2020 na 2021) hatukutoa tuzo hizi kutokana na janga la UVIKO-19, ninawaomba waajiri wote wajitokeze kwa wingi kushiriki katika mchakato huu muhimu wa kumtafuta mwajiri bora wa mwaka 2022 ambaye atatangazwa mapema mwezi Desemba mwaka huu," alisema.

Alisema wataendelea kuwa na tuzo ya mshindi wa jumla na ile ya kulingana na ukubwa wa kampuni au taasisi.

"Kutakuwa na tuzo ya waajiri bora katika sekta binafsi, tuzo ya sekta ya umma, tuzo ya mashirika ya ndani ya nchi na tuzo ya mashirika yasiyo ya kiserikali na tuzo ya maudhui ya ndani," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema kitabu kilichorekebishwa cha mwongozo wa misingi muhimu ya kusimamia rasilimali watu ya tuzo ya mwajiri bora wa mwaka kitakuwa tayari hivi karibuni na kuwataka waajiri waweze kujipatia.

Alisema mwongozo huo ulioandaliwa utakuwa na madhumuni ya kushawishi, kuelimisha na kusaidia wanachama wa ATE umuhimu wa rasilimali watu, mifumo na stadi zinazohitajika kujenga taasisi imara.

# Mbaroni madai kumuua mtoto wa mdogo wake kisha kumtupa mtoni

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, linamshikilia Latifa Bakari (33) mkazi wa Mabibo kwa tuhuma za mauaji ya mtoto wa mdogo wake mwenye umri wa miaka miwili.

Mtuhumiwa huyo, mkazi wa Mabibo, Dar es Salaam, anadaiwa kuutupa mwili katika mto ulioko Ubungo Riverside.

Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi (ACP) Jumanne Muliro, alisema jana kuwa Latifa aliachiwa mtoto huyo na mdogo wake kwa lengo la malezi na Aprili 5, mwaka huu, alifanya mauaji hayo baada ya kumpiga mtoto huyo kupita kiasi.

Alisema mtuhumiwa alipobaini kuwa mtoto huyo amefariki dunia baada ya kumpiga, Aprili 6, mwaka huu, aliukunja mwili wa mtoto na kuuweka kwenye ndoo ya plastiki kisha kuutumbukiza kwenye kiroba na kwenda kuutupa mtoni eneo la Riverside.

"Baada ya majirani kutomwona mtoto huyo kama ambavyo si kawaida, walitoa taarifa polisi na alipohojiwa kwa kina, mtuhumiwa alikiri kufanya mauaji hayo na kwenda kuwaonyesha Polisi mwili wa mtoto huyo ulipokuwa," alisema Muliro.

Kamanda Muliro aliongeza kuwa mwili wa marehemu umepelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa uchunguzi zaidi na mtuhumiwa atafikishwa mahakamani baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Katika hatua nyingine, Muliro alibainisha kuwa jeshi hilo limewakamata Omary Ally (28) mkazi wa Tegeta na Juma Sulleiman (30) mkazi wa Wazo, kwa tuhuma za kuharibu na kuhujumu miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) zikiwamo nyaya aina ya shaba kwa lengo la kuziuza.

Wengine ni wanunuzi wa vifaa hivyo, Amos John (30) mkazi wa Tegeta na Mokolo Machage (26) mkazi wa Bunju ambao walikamatwa Aprili 10 na baada ya kuhojiwa walikiri kuhusika na matukio hayo. Alisema walipopekuliwa katika maeneo yao walikutwa na viroba vinne vya nyaya hizo zikiwa zimechunwa.

"Jeshi la Polisi linaendelea kutoa onyo kuwa halitamvumilia mtu au kikundi chochote kinachojihusisha kwa namna yoyote ile kujaribu kuharibu miundombinu ambayo imejengwa kwa manufaa ya umma. Atakayejaribu atakamatwa na taratibu za kumfikisha kwenye vyombo vya sheria zitazingatiwa," alisema Muliro.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bila uwajibikaji madudu ripoti ya CAG hayataisha

**JANA** ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ilikabidhiwa kwa Bunge ambayo sasa itakuwa wazi kwa umma kusoma na kujua kilichopo ndani.

Katika ukaguzi wake kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), CAG alibaini watu 444 walipimwa kipimo cha damu zaidi ya mara moja, huku wengine wakipimwa zaidi ya mara 30 kwa siku moja.

Aidha, wanaume 731 walionekana wamepewa huduma za kujifungua jambo ambalo linatia shaka, na kuzua maswali mengi juu ya matumizi ya fedha za umma.

Kwa ujumla ripoti inaonyesha wapi pametoboka serikalini kiasi cha fedha kutoka kwenda kwenye mikono ya watu, badala ya kuhudumia wananchi ambao ndiyo walipa kodi.

Kila mwaka ripoti ya CAG inaonyesha upigaji ambao kimsingi unakatisha tamaa walipakodi, kwamba fedha zao hazitunzwi na kutumika kwenye miradi inayotakiwa ambayo italeta tija kwenye maisha yao. Pia, alibaini kuwa miradi ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha za mikopo haikukamilika kwa wakati, ambayo moja kwa moja inagusa maisha ya watu jambo linaloonyesha inapaswa kufuatiliwa kwa karibu utekelezaji wake.

Kwenye halamshauri madudu yameendelea kuonekana ikiwamo uchepushaji wa fedha nyingi kutoka hazina kwenda maeneo hayo kuliko kiasi kilichotakiwa, jambo ambalo linakatisha tamaa kwa kuwa wananchi wanatarajia kupata huduma muhimu.

Wakati hali ikiwa hivi walipakodi ndiyo wanatibiwa kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma ambazo kila mara wanaambiwa hakuna dawa au vifaa tiba, huku wengine wakitembea umbali mrefu kutafuta huduma hizo.

Lakini ndiyo wanateseka kuyafikia masoko kutokana na miundombinu duni kwa kuwa hakuna fedha za kujenga barabara ili wasafiri bila kikwazo, lakini ndiyo hao ambao watoto wao wanakosa elimu nzuri kwa kuwa hakuna madawati au vyumba vya madarasa vya kutosha.

Pia, ndiyo hao wanaokosa maji wanalazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji huku wanawake na wasichana wakipata madhila ya kubakwa au kufanyiwa vitendo vibaya, lakini hao hao wanasikia fedha zimechotwa na watu fulani.

Ni lazima kujenga mifumo ya uwajibikaji kuzuia fedha za umma kupenya kwenye mkondo usio sahihi, kwamba isizoeleke kuwa kuiba ni jambo la kawaida. Ni muhimu watumishi wa umma wakatenda majukumu yao kwa hofu ya Mungu ndani yao kwa kutambua kuwa nafasi walizopewa ni dhamana na ipo siku mbele ya muumba wataulizwa kama walitimiza wajibu wao ipasavyo.

Kwa Mtanzania maskini asiye na uhakika wa kesho atakula nini anaposikia fedha zimechotwa kwenye mradi ambao ungebadilisha maisha yake ni kuendelea kumsononesha na kutokuwa na huruma kwa kuwa huenda kuna waliofariki kwa kukosa dawa au huduma muhimu za afya.

Leo hii huduma za afya kwenye vituo vya huduma vya serikali siyo za kuridhisha kiasi cha wengi kukimbilia sekta binafsi, lakini ilipaswa kila mmoja kukimbilia huduma za umma kwa kuwa ni nzuri, za uhakika na nafuu kama nchi zilizoendelea.

Ukisikiliza wabunge kila mara wanauliza maswali ya lini serikali itafanya hili na hili au kutoa fedha za kutekeleza mradi fulani ambao unategemewa na wananchi fulani, jibu huwa ni kwamba mchakato unaendelea na fedha itakapopatikana utajengwa, lakini wakati huo huo kuna watu wamefuja fedha za umma na kumanufaa yao.

Kwa nchi zilizoendelea hawazungumzii tena huduma za afya kama jambo la gharama bali ni bure kuanzia elimu, afya na miundombinu kwa kuwa walitumia fedha zao vizuri kuhakiksiha zinajengwa, lakini ni kashfa na kosa kubwa kwa mtu kukwepa kodi au kuiba fedha au mali ya umma.

Wapo waliowajibishwa ikiwamo kuondolewa madarakani kwa sababu ya kubainika kutumia vibaya mali ya umma, lakini kwa nchi za Afrika inaonekana ni kawaida kwa kuwa upo mtandao wa kulinda ulaji kuendelea, jambo ambalo linapaswa kukemewa ili kuboresha maisha ya watu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ama kweli jamani tumuenzi Nyerere kwa matendo yetu

Na Adam Fungamwango

**LEO** Aprili 13, Watanzania tunaadhimisha miaka 100 tangu kuzaliwa Baba wa Taifa, Rais wa Kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Pamoja na vyeo vyote na nyadhifa mbalimbali nchini, lakini mwenyewe alipenda kujiita zaidi kama Mwalimu, akiwa na maana halisi ya kazi yake kitaaluma ya ualimu.

Nyerere aliyezaliwa Aprili 13, 1922 kwenye kijiji cha Butiama, mkoani Mara, alifariki dunia Oktoba 14 hospitalini nchini Uingereza mwaka 1999 alikokuwa anatibiwa.

Ina maana kama angekuwa hai hadi leo hii, angekuwa anatimiza miaka 100. Nina uhakika kuwa si Watanzania tu ambao watakuwa wanaadhimisha hilo, bali hata mataifa mengine ya nje ambayo kwa kiasi kikubwa uhuru wao ulichangia mno.

Moja kwa moja ni Tanzania chini ya mawazo ya Mwalimu na maneno yake kuwa "Tanzania haiwezi kuwa huru, kama nchi nyingine za Afrika hazijawa huru."

Nchi hizo ni kama Msumbiji, Namibia, Zimbabwe, na Afrika Kusini, huku Uganda nayo ikikumbuka jinsi ilivyoteseka chini ya utawala dhalimu wa Idd Amin Dada, kabla ya kung'olewa chini ya majeshi shupavu ya Tanzania, yaliyoongozwa na Hayati Mwalimu Nyerere.

Tumeona makongamano mbalimbali kukumbuka na kuenzi yale yaliyofanywa na hayati Mwalimu Nyerere.

Kila mtu angependa kuendeleza na kuishi kwa yale ambayo Nyerere aliyafanya kuanzia viongozi hadi watu wa hali ya chini, ingawa wakati mwingine ni ngumu sana.

Kuna wakati Nyerere unaweza kumtafsiri hakuwa na kipawa cha kawaida, achilia mbali akili yake, uwezo wa kupambanua mambo, kujieleza, kutoa hotuba isiyochosha hata akizungumza saa kumi ana ushawishi.

Pia, aliishi kwa kile ambacho alikuwa akikizungumza na si vinginevyo. Hakuwa mtu wa majivuno na kujikweza, licha ya kwamba hakuwa kiongozi anayeheshimiwa nchini Tanzania tu, bali Afrika nzima na dunia kwa ujumla.

Ni Nyerere huyo huyo ambaye kuna wakati alikuwa Mwenyekiti wa Nchi Zilizo Mstari wa Mbele za Ukombozi Kusini mwa Afrika, lakini mavazi yake na utakapomkuta wakati mwingine kijijini kwake Butiama, unaweza kukataa kuwa si yeye.

Viongozi wengi waliomfuata Butiama, walimkuta shambani akilima tena kwa jembe la mkono, kitu ambacho kiliwashangaza wengi.

Halafu vilevile kabla ya kuwakaribisha nyumbani kwake na kusema kilichowapeleka, aliwapa elimu kwanza ya kilimo huko huko shambani ambako mwenyewe alipenda wapelekwe kwanza kumtembelea huko, badala ya kumsubiri nyumbani.

Kiongozi aliyekuwa mfuasi wa siasa ya ujamaa, aliishi kijamaa hivyo hivyo, tofauti na hata baadhi ya viongozi wa baadhi ya nchi za nje ambao ujamaa wao ni kwenye mdomo na kwenye makaratasi, lakini nyuma ya pazia, walikuwa wamelimbikiza mali.

Hadi anafariki, hadi leo hapajawahi kuzuka hata tetesi kuwa alikuwa akimiliki mali za ajabu,, achilia mbali, mali zingine, kampuni au viwanda.

Nyumba alijengewa siku zake za mwisho na hakuishi muda mrefu, akafariki. Hakika alikuwa mjamaa wa kweli.

Kingine alikuwa na utu. Alipenda binadamu wote wawe sawa. Hakupenda hata yule ambaye amemzidi mwenzake kwa kipato amnyanyase mwenzake.

Akahakikisha mwananchi ambaye hana uwezo wa kununua kidonge cha dawa, anatibiwa hospitalini bila matatizo.

Akasomesha watoto wa masikini bure, ambao hata ingekuwaje, kwa uwezo wa wazazi wao wasingeweza kupata elimu walizo nazo sasa.

Wanafunzi hawakulazimika kununua madaftari shuleni, badala yake kila lilipomalizika, mwalimu anatia saini na linakwenda kuchukuliwa stoo, pamoja na kalamu.

Ukitaka kumzungumzia Nyerere, unahitaji kujaza kurasa na kurasa, kwa sababu alikuwa na mambo mengi aliyoyafanya ya kuzungumziwa kwenye uongozi wake nchini, nje ya nchi, na hata shughuli zake zingine baada ya kazi, kama vile kucheza bao, na kuandika vitabu mbalimbali.

Ni kiongozi ambaye taifa la Tanzania limepata bahati ya kujivunia kuwa alizaliwa kwenye nchi yake.

Ni kiongozi aliyewashangaza hata viongozi wa mataifa makubwa, wakiwamo waliompinga na hata maadui zake.

Kinachopaswa kwa Watanzania wote wa ngazi mbalimbali, inafaa tumuenzi kiongozi huyu kwa vitendo, hasa kwa kuwa Wazalendo kwenye nchini yetu kama ambavyo yeye alivyolifanya taifa liwe wakati huo, kiasi kwamba hadi sasa limekuwa kama Taifa la familia moja, lisilo la ukabila wala udini.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TANGAZO LA KUITWA KAZINI

**Dar es Salaam, 12 Aprili, 2022:**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwataarifu waombaji wa nafasi za kazi waliofaulu usaili na kupewa barua za ajira na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma na kisha kupangiwa kujiunga na TRA kama kituo chao cha kazi, kufika katika Chuo cha Kodi (ITA) kilichopo ITV Mikocheni – Eneo la Viwanda Dar es Salaam mnamo **tarehe 19 Aprili, 2022 saa 1:30 asubuhi** bila kukosa.

Wahusika hao wanatakiwa kufika ITA wakiwa na nyaraka zifuatazo: -

1. Barua ya kupangiwa kituo cha kazi kutoka Sekretarieti ya Ajira;
2. Kiapo kilichothibitishwa na Msajili wa Hati *(Deed poll)* kutoka Wizara ya Ardhi endapo muhusika aliwahi kubadilisha majina;
3. Vyeti vya kuhitimu elimu na taaluma;
4. Nyaraka zote muhimu za taarifa binafsi, ziwe na majina matatu ya muhusika mfano cheti cha kuzaliwa na vyeti vya taaluma. Endapo jina mojawapo halipo katika vyeti basi atahitajika kuwa na kiapo kilichothibitishwa na Msajili wa Hati *(Deed poll)* kutoka Wizara ya Ardhi.
5. Kwa waliosoma nje ya nchi kwa elimu ya sekondari na vyuo wawasilishe nakala za uthibitisho kutoka NECTA, NACTE na TCU;
6. Cheti cha Kuzaliwa *(Birth Certificate)* cha mwajiriwa pamoja na wategemezi (Mme/Mke/Watoto) kama mhusika ameoa au kuolewa;
7. Cheti halisi cha ndoa kama mhusika ameoa au kuolewa;
8. Kitambulisho cha Taifa (NIDA);
9. Picha ndogo ya sasa *(Current Passport size)* yenye rangi ya bluu nyuma yake *(Blue background)*;
10. Leseni halisi ya udereva Daraja C iwapo muhusika ameajiriwa kama Dereva.
11. Kwa watumishi wanaohamia kutoka taasisi nyingine za Serikali/Umma wanatakiwa kuwasilisha pia nyaraka zifuatazo zikiwa zimethibitishwa kwa sahihi na muhuri wa mwajiri wa awali.

**i)** Barua ya ajira kutoka kwa mwajiri wa awali;
**ii)** Barua ya kuthibitishwa kazini kutoka kwa mwajiri wa awali;
**iii)** Barua ya kupandishwa vyeo kutoka kwa mwajiri wa awali;
**iv)** Taarifa za madeni, kama yapo;
**v)** Taarifa za uhakiki wa matokeo ya kidato cha nne;
**vi)** Fomu ya taarifa binafsi *(Personal records form)* aliyoijaza kwa mara ya kwanza kwa mwajiri wa awali;
**vii)** Fomu ya taarifa za utumishi *(Service particulars form)* kutoka kwa mwajili wa awali.

Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo;

| | |
|---|---|
| Tovuti | : **www.tra.go.tz** |
| Namba za simu bila malipo | : **0800 780078 au 0800 750075** |
| WhatsApp | : **0744 23 33 33** |
| Barua pepe | : **huduma@tra.go.tz** au **services@tra.go.tz** |

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:
**Idara ya Rasilimali Watu na Utawala**

# Abood aipa mbinu serikali tatizo ajira

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAKATI tatizo la uhaba wa ajira nchini 'likiteka' mijadala ya Bunge kwa takriban wiki mbili sasa, Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdul-Aziz Abood (CCM), amesema kilimo cha umwagiliaji ni miongoni mwa njia nyepesi ya kutatua tatizo la ajira kwa vijana nchini.

Abood alibainisha hayo bungeni jijini hapa juzi jioni wakati wa mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/23, akisema Tanzania ina kila uwezo mkubwa wa kufanya kilimo cha umwagiliaji.

"Nimesikia wabunge wengi wakizungumzia kilimo na tatizo la ajira. Tatizo kubwa lililopo ni vijana kukosa ajira lakini njia fupi na nyepesi duniani kote ya kuondoa uhaba wa ajira ni kilimo, hasa cha umwagiliaji," alisema.

Abood alisema Tanzania ina maziwa na mito, hivyo kuwa na uwezo wa kujenga mabwawa makubwa yatakayokinga maji ya mvua ili kuwezesha kilimo ch umwagiliaji.

Mbunge huyo alisema Tanzania inaweza kuwa mzalishaji mkubwa wa kilimo cha mpunga kusini mwa Afrika na barani Afrika kwa ujumla endapo itaitumia vyema ardhi yenye rutuba iliyonayo.

"Morogoro kuna eneo linafaa kwa umwagiliaji hekta zaidi ya milioni moja, lakini linalotumika kwa sasa ni hekta 40,558. Ninaishauri serikali tukijikite katika upande huu ili kutoa ajira nyingi kwa vijana," alisema.

Kuhusu kero za kijamii jimboni kwake, Abood alisema wananchi wanakabiliwa na shida katika upatikanaji wa maji, akitaka serikali kuchukua hatua ili kuitatua.

Abood alisema shida hiyo ipo kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wenye gharama ya Sh. bilioni 180.

**KABOYOKA NA MIFUGO**

Katika mjadala huo, Mbunge wa Viti Maalum, Naghenjwa Kaboyoka (CHADEMA), aliitaka serikali kuwekeza kikamilifu kwenye Sekta ya Kilimo.

Alisema Tanzania ni nchi ya tatu barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo, ikiwa na ng'ombe milioni 25 kwa sasa. lakini mchango wa sekta hiyo kwenye Pato la Taifa ni mdogo.

Alisema Kenya wenye ng'ombe milioni 21 wanapata fedha nyingi kutokana na uwekezaji mkubwa walioufanya kwenye eneo hilo, sawa na Denmark wenye ng'ombe milioni 1.5.@

"Asilimia 98 ya ng'ombe wetu ni wa kienyeji na wanafugwa kienyeji. Ukiiangalia Denmark ambayo ina ng'ombe milioni 1.5, wana kipato kikubwa kwenye mifugo.

"Hivi Tanzania tutangoja hadi lini wananchi wetu wanaendelea kuumia? Yaani nchi yetu iko tayari kufanya lolote kuwezesha maendeleo ya migodi lakini haiko tayari kufanya lolote kuwezesha maendeleo ya mifugo," alilalamika.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (katikati), akipokea hati ya makabidhiano ya ofisi kutoka kwa aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Mahusiano na Serikali na Msemaji wa benki hiyo, William Kallaghe (kulia), jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kallaghe, amestaafu utumishi wa benki hiyo, huku nafasi yake ikichukuliwa na Godwini Semunyu (kushoto). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NICOL yaita wanahisa kuteta jambo lao

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya Uwekezaji ya National Investment Company Limited (NICOL) imeitisha Mkutano Mkuu Maalum wa wanahisa wake kwa ajili ya kupitisha wakurugenzi wapya waliochaguliwa hivi karibuni.

Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Erasto Ngamilaga, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu mafanikio ya kampuni hiyo.

Alisema ongezeko hilo la wakurugenzi linatokana na azimio la wanahisa lililotolewa kwenye mkutano mkuu wa saba uliofanyika Desemba, mwaka jana.

Ngamilaga alisema kwenye mkutano huo, ilikubaliwa idadi ya wakurugenzi iongezeke mpaka kufikia saba na taratibu zifuatwe kwa wakurugenzi ambao muda wao ulifika kikimo.

"Mkutano utaanza saa mbili asubuhi tunawaomba wanahisa watakaohudhuria mkutano huo kuwahi mapema na wote watakaopenda kuhudhuria kwa njia ya mtandao wajisajili mapema. Taarifa za namna ya kuingia kwenye mtandao wanahisa watatumiwa kwenye simu zao," alisema.

Baada ya mkutano huo wa saba, alisema kampuni iliendelea kutekeleza maazimio hayo kwa kutangaza nafasi hizo na baada ya kukamilika kwa mchakato wa usahili huo majina na sifa za wakurugenzi hao yalitangazwa kwenye vyombo vya habari kuwajulisha wanahisa.

"Sasa kwa mujibu wa taratibu wakurugenzi hao wakipatikana wanastahili kupitishwa na Mkutano Mkuu wa wanahisa, hivyo kwa kuzingatia sheria, mkutano mkuu maalum wa wanahisa umeitishwa ili kuwapitisha kwa kuwapigia kura wakurugenzi hao," alisema

"Mkutano utafanyika kwa njia mbili, kwa njia ya mtandao kwa watakaoshindwa kufika na wanahisa watakaoweza kufika kwenye mkutano wafike Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es Salaam. Ajenda itakuwa moja tu kupitisha wakurugenzi kwa kuwapigia kura na baada ya hapo NICOL itakuwa imepata wakurugenzi kwa mujibu wa sheria," alisema.

Alitaja sababu ya kuomba kuongeza idadi ya wakurugenzi ni kutokana na mikakati mikubwa ya ukuaji ya miaka mitano ambayo kampuni imejiwekea hivyo ili kufanikisha maono hayo kampuni inahitaji kuwa na wakurugenzi wenye maono ya uwekezaji na usimamizi bora wa kampuni.

Kuhusu mafanikio ya kampuni hiyo, alisema NICOL imeendelea kufanya vizuri kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na hisa zake zimepanda kutoka bei ya Sh 170 mwaka 2021 hadi kufikia Sh 580 Aprili, mwaka huu, na kwamba mafanikio hayo yanatokana na jitihada kubwa zilizofanywa na uongozi.

Alisema NICOL imefanya mtawanyo wa uwekezaji kwa kuwekeza kwenye maeneo yenye tija ambapo uwekezaji kwenye hati fungani pekee kampuni imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 15.

Menejimenti ya kampuni hiyo, alisema imejitahidi kupunguza gharama za uendeshaji hali ambayo imesababisha ongezeko la faida baada ya kodi kufikia Sh. bilioni nne mwaka 2021.

# Jotoardhi kuongeza umeme megawati 200

**Na Salome Kitomari**

MIRADI minne ya kuzalisha umeme wa joto ardhi inatarajiwa kukamilika 2025 na kuzalisha megawati 200 ambazo zitaingizwa kwenye gridi ya taifa kwa ajili ya matumizi.

Kwa mujibu wa wasilisho la Taasisi ya Uendelezaji Jotoardhi Tanzania (TGDC), miradi hiyo na kiasi cha umeme ni Ngozi (75), Songwe (5), Kiejo-Mbaka (60) na Luhoi (5) ambayo ipo hatua ya uhakiki wa rasilimali kwa kuchoronga visima, huku Mradi wa Ziwa Natron ukitarajiwa kuzalisha Megawati 60.

Tarafa hiyo ilibainisha kuwa mradi wa Kiejo –Mbaka kinachoendelea ni uchorongaji wa visima vifupi huku programu ya uchorongaji wa visima vya uhakiki kwa mradi wa Ngozi ikiendelea pia, pamoja na miradi ya majaribio ya matumizi mengine ya jotoardhi ikiendelea kutekelezwa eneo la Songwe.

Aidha, TGDC inasema uwezo wa rasilimali ya jotoardhi nchini ni kuzalisha umeme wa megawati 5,000 katika maeneo 52 kwenye mikoa 16 nchini na idadi ya maeneo kwenye mabano ni Arusha (5), Dodoma (4), Iringa (1), Kagera (1), Morogoro (3), Mbeya (6), Kilimanjaro (2), Katavi (1), Shinyanga (1), Songwe (2), Manyara (5), Rukwa (2), Singida (3), Pwani (2) na Tanga (3).

Pia, imeeleza hatua za uendelezaji jotoardhi ni utafiti ambao hujumuisha wa awali na kina juu ya ardhi kuangalia jiolojia, jiofizikia, jiokemia, ya pili ni uhakiki wa rasilimali kwa kufanya tathmini ya kimazingira, uchorongaji wa visima vya uhakiki, upembuzi yakinifu wa awali na tatu ni uendelezaji na uzalishaji kwa uchorongaji visima vya uzalishaji, ujenzi wa mitambo uzalishaji na uendeshaji na uangalizi.

Mtaalam kutoka TGDC, alisema matumizi ya jotoardhi ni pamoja na kuzalisha umeme wa kuendesha mitambo, kitalu nyumba kwa ajili ya kukaushia mazao, mabwawa ya kuogelea ambayo hutumika kama tiba ya mwili na utalii na ufugaji na ukaushaji wa samaki na kuku.

Kwa duniani nchi 90 zina maeneo yenye jotoardhi, kati yake 26 zinazalisha jumla ya gigawati 15.6 za umeme wa joto ardhi, na kwamba kwa Afrika, Kenya inaongoza kwa kuzalisha nishati hiyo zaidi ya megawati 890.

## Sengerema yapigwa jeki chanjo UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Sengerema mkoani Mwanza, imekabidhiwa vipaza sauti kutoka kampuni ya Madini ya OreCorp Tanzania Limited, ikiwa ni jitihada za kuhamasisha kampeni ya kujenga ufahamu wa chanjo dhidi ya Uviko-19.

Makabidhiano hayo ni moja ya mipango ya kijamii inayofanywa na OreCorp kuisaidia wilaya ya Sengerema kwenye kampeni ya kujenga ufahamu wa chanjo dhidi ya UVIKO-19.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga, akipokea vifaa hivyo kutoka kampuni hiyo jana, alisema vitatumika katika shughuli zijazo za wilayani humo ikiwamo kuunga mkono jitihada za kuishi na afya bora na kupunguza athari zitokanazo na Uviko-19 na maradhi mengine.

Alisema mpango huo unajumuisha kufanya kazi pamoja ofisi ya Ofisa Afya wa Wilaya kutoa taarifa fupi za kila mwezi kuhusu faida za chanjo katika mradi wa dhahabu wa Nyanzaga, ikiwamo kuweka kituo cha chanjo kwenye mgodi huo.

"Vipaza sauti na spika hizo vitatumika kwenye hafla za namna hiyo na programu zingine zitakazoendeshwa na Wilaya ya Sengerema. OreCorp inajidhatiti kuhakikisha wafanyakazi wake, washauri na wageni wa mgodini wanafahamu hatari itokanayo na Uviko-19 na kupima kiwango cha joto na kunawia mikono," alisema mkuu wa wilaya huyo.

Meneja Mkuu wa kampuni hiyo, Damien Valente alisema kuwa, OreCorp inafurahia ushirikiano endelevu uliopo na Wilaya ya Sengerema katika maeneo yote ya maendeleo ya jamii, akisema mradi uko mbioni kuwa mgodi mkubwa zaidi wa kwanza wa dhahabu kuwahi kujengwa.

"Mradi wa dhahabu wa Nyanzaga upo Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza kwenye ukanda wa dhahabu wa Ziwa Victoria. Mradi wa Nyanzaga unakadiriwa kuwa na wakia milioni tatu za dhahabu na utazalisha kiasi cha wakia 200,000 (tani sita) za dhahabu kwa mwaka na ujenzi wake ni shilingi bilioni 670.

"Mradi huu utazalisha nafasi za ajira muhimu na kuchangia uchumi kupitia ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, mirabaha na kodi, utaleta faida za ziada kwa Mkoa kama vile elimu, vituo vya afya na miundombinu kupitia miradi wezeshi inayofanywa na kampuni hiyo kwa lengo la kuinufaisha jamii," alisema Valentene.

Aliongeza kwamba, kampuni hiyo itaendelea kufanya kazi ngazi zote za serikali ili kuhakikisha inatimiza ujenzi wa mgodi wa madini ya dhahabu kwa Watanzania na wadau wake wote katika kipindi cha zaidi ya miaka 10.

# Waitara alia mil. 900/- kubadilishiwa matumizi

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MBUNGE wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara (CCM), amelalamikia kile alichodai kubadilishwa kwa matumizi ya Sh. milioni 900 zilizotolewa na Mgodi wa Dhahabu wa Barrick North Mara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo.

Vilevile, amelalamikia kamati ya mawaziri wanane kutomshirikisha katika utatuzi wa mgogoro wa ardhi jimboni, akisisitiza kuwa hatakubali bomu analotegeshewa limlipukie yeye mwenyewe.

Waitara aliyasema hayo bungeni alipochangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema kuwa halmashauri ilipitisha fedha hizo zitumike kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo hususan kwenye maeneo yanayouzunguka mgodi huo, lakini uongozi mpya wa Mko wa Mara umebadili matumizi ya fedha hizo. Pia alisema kuwa tangu mwaka 2020, alimwomba aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, aende katika Jimbo la Tarime Vijijini kwenye kata za Nyanungu, Kihacha na Nyarukoba lakini hakwenda.

Alisema anamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuunda kamati ya mawaziri wanane, wakazunguka huko kuangalia maeneo yenye shida ya migogoro ya ardhi lakini wakaishia Musoma mjini pasi na kuzuru jimboni kwake.

Alisema juzi Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula na Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, walitoa tamko mjini Musoma na aliwauliza wabunge wenzie iwapo wameshirikishwa na wakamjibu kwamba hawakushirikishwa.

Alisema kuna watumishi kutoka wizara hizo wamekwenda Tarime na kuonyesha wakazi waliokuwa kwenye vijiji vyenye mgogoro maeneo ambayo tayari yana vijiji ambavyo watu wanaishi.

Alisema kinachomuuma ni kwamba watu hao walisema yeye ameshirikishwa kwenye uamuzi huo katika kijiji cha Nanyungu ambacho wananchi walimpigia kura wakati wa uchaguzi mkuu na yeye akawaahidi atawatetea.

Alimwomba Waziri wa Maliasili na Utalii na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi waende Mkoa wa Mara ambao una migogoro ya ardhi.

Alitaka ujumbe huo uwafikie mawaziri wengine na kwamba yeye hana ugomvi nao na anachomaanisha ni kuwa wanaweza kutengeneza hoja nzuri na wabunge walio katika maeneo yenye migogoro ya ardhi wakashinda katika uchaguzi.

"Mnaniwekea bomu, nitakubali tulipuke wote siyo mimi pekee yangu," Waitara alisema huku akiongeza kuwa ripoti ya uchafuzi wa Mto Mara imeleta shida kwenye jimbo lake kwa kuwa wakazi wa maeneo hayo wamekataa kutumia maji ya mto huo.

Hata hivyo, baada ya kumaliza kuchangia, Naibu Spika, Mussa Zungu, alimwambia Waitara kuwa alipokuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), alikuwa anakwenda katika migodi bila kuwaambia wabunge wenzake.

Alisema pia alipokuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, alikuwa anakwenda kwenye miradi ya barabara bila kuwashirikisha wabunge wa maeneo husika.



Meneja wa kiwanda cha SBL Moshi, mkoa wa Kilimanjaro, Alice Kilembe (wa tano kulia), akiwa na baadhi ya wanafunzi wa chuo cha kilimo Kilacha, baada ya kupokea vyeti vyao vya ufadhili wa masomo kupitia programu ya SBL Kilimo Viwanda, mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muhongo ataja ilipo dawa tatizo la ajira

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

MBUNGE wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo (CCM), ameungana na wabunge wengine kuitaka serikali kuwekeza fedha nyingi katika kilimo, akiamini ndiyo njia sahihi ya kukabiliana na tatizo la uhaba wa ajira nchini. Akichangia bungeni mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha, Prof. Muhongo pia alisema taifa linapaswa kuwa na sera nzuri ya maendeleo ya utafiti na ubinifu.

Alikumbusha kuwa nchi za Afrika mwaka 2006 zilipitisha azimio la kutenga walau asilimia moja ya Pato la Taifa kutumika kwenye utafiti, lakini nchi nyingi hazijafika huko, Tanzania ikitumia asilimia 0.5 asilimia ya Pato la Taifa.

Kwa hiyo, mpango wa utafiti na programu za shahada zetu lazima tuwekeze huko.

"Eneo lingine ni sayansi ya maisha, sayansi ya nyuklia, sayansi ya mazingira na 'artificial intelligence'. Tukitaka kufanya haya ni lazima COSTECH ibadilike, isiwe idara ndogo, ni lazima tutengeneze kitu kinaitwa National Reserch Foundation and Innovation," alishauri.

Prof. Muhongo alisema kilimo, uvuvi na ufugaji ndiyo maeneo yatakayotengeneza ajira nchini na siyo kutegemea ajira za serikali.

"Tulime mazao yanayopendwa duniani ambapo vyakula vinavyopendwa duniani kwa sasa ni 12 ambavyo ni poamoja na salad, wali, kahawa, mayai, apples (tufani), yoghurt, mkate, supu. Tuwe na mpangilio wa kuzalisha ili kuiuzia duniani na ili kufanikisha hili, ni lazima tufanye kilimo cha umwagiliaji.

Mbunge wa Viti Maalum, Munde Tambwe (CCM), alisema serikali inapaswa kutilia mkazo kilimo cha alzeti na mazao mengine yanayotumika kuzalisha mafuta ili kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuagiza mafuta nje ya nchi.

Selemani Kakoso (Mpanda Vijijini),, aliitaka serikali kuja a na mkakati wa uwekezaji kwenye kilimo cha umwagiliaji, utafiti wa mbegu na kuajiri wataalamu wa kilimo.

Jason Rweikiza (Bukoba Vijijini)), alisema nchi ina maeneo yenye rutuba na mito mingi inayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lakini ina vijana wengi ambao hawana kazi, akipendekeza kuanzishwe kambi za kilimo ili kukabiliana na uhaba wa ajira kwa vijana.

# Serikali zachukua hatua kuvilinda visiwa

SERIKALI ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimechukua hatua tatu katika kukabiliana na uharibifu unaotokana na ukataji mikoko na uvunaji wa matumbawe ili kuvinusuru visiwa visitoweke katika uso wa dunia.

Hatua hizo ni pamoja na kujenga uelewa kwa wanajamii juu ya utunzaji wa mazingira na rasilimali za bahari ikiwamo uhifadhi wa mikoko na matumbawe.

Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Wete(ACT), Omar Ali Omar. Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua serikali imejipangaje katika kukabiliana na uharibifu huo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chilo alisema serikali hizo mbili zimekuwa zikichukua juhudi za kisera, kisheria na pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali ya utunzaji wa mazingira ya baharini ili kuhakikisha uharibifu wa mazingira ya bahari unadhibitiwa.

Alitaja juhudi nyingine kuwa ni upandaji wa mikoko na Matumbawe katika maeneo yaliyoathirika kwa kutumia njia mbalimbali endelevu na za kitaalamu.

"Juhudi nyingine ni kushirikisha jamii katika kusimamia maeneo ya mikoko na matumbawe ikiwemo kuanzisha hifadhi ndogo ndogo za Kijamii katika maeneo ya Kukuu, Fundo, Makoongwe kwa kisiwa cha Pemba na maeneo ya Mtende, Tumbatu na Kizimkazi kwa kisiwa cha Unguja," alisema.



Mbunge wa Jimbo la Morogoro, Azizi Abood, akichangia hotuba ya Waziri Mkuu ya Mwaka wa fedha wa 2022/2022, kwenye kikao cha Bunge la bajeti, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Kanzidata ya NIDA kuboresha daftari la wapigakura

BUNGE limeelezwa kuwa serikali mwezi uliopita ilianza mazungumzo na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC),na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ili kanzidata ya NIDA itumike katika uboreshaji wa daftari la wapigakura.

Aidha, mazungumzo ya awali kati ya wataalam wa taasisi zote mbili yenye nia ya kuunganisha mifumo hiyo miwili yamepangwa kufanyika kabla ya mwezi Mei, 2022.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais,Muungano na Mazingira Khamis Hamza Chilo alieleza hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kawe(CCM), Askofu Josephat Gwajima, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua serikali haioni umuhimu wa kuunganisha mifumo ya kitambulisho cha mpiga kura na kitambulisho cha taifa ili kuepusha usumbufu kwa wananchi.

Akijibu swali hilo, Chilo alisema serikali inatambua umuhimu wa kuunganisha mifumo ya Kitambulisho cha Mpiga Kura na Kitambulisho cha Taifa ili kutumia Kitambulisho cha Taifa katika Uchaguzi wa kawaida na ule wa kielektroniki 'e-voting .

Alisema hatua hiyo itapunguza gharama katika kuandikisha na kutengeneza daftari pamoja na kurahisisha usimamizi wa wapiga kura.

Aidha alisema matarajio ya serikali ni kuona mifumo hiyo inaunganishwa ili kuwarahisishia wananchi kushiriki katika shughuli za uchaguzi na kuipunguzia serikali gharama katika uandikishaji na uchapishaji wa vitambulisho.




Habari zote na Augusta Njoji

# Bashe: Walionunua mbegu zisizo na ubora watoe taarifa

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe amesema kama kuna mtanzania amenunua mbegu zisizo na ubora atoe taarifa kwenye wizara hiyo na hatua zitachukuliwa kwa kuwa ni uhujumu uchumi.

Bashe alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM),Noah Mollel aliyetaka kujua juu ya mikakati ya serikali kusimamia ubora wa mbegu kutokana na kuwapo kwa malalamiko kuhusu ubora wa mbegu.

Alisema kuna kesi ipo Mkoa wa Ruvuma ambayo mtu aliuza mbegu aliziwekea rangi na amepelekwa Mahakamani ili kuchukuliwa hatua kwa kuwa ni uhujumu uchumi na halitafumbiwa macho.

Katika hatua nyingine, Bashe alisema serikali imeweka utaratibu wa kudhibiti upandishaji holela wa bei za mbolea kwa kuhusisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania(TFRA) na Mikoa kwa kufanya tathmini ya gharama halisi ya bei ya mbolea kwa mkulima na kutoa bei elekezi.

Hatua hiyo itadhibiti upandaji wa bei unaofanywa na wafanyabiashara bila kuzingatia gharama halisi za uingizaji wa mbolea nchini.

Akijibu swali la Mbunge wa Namtumbo(CCM),Vita Kawawa aliyetaka kujua serikali inachukua hatua gani kudhibiti kuongezeka kwa bei ya mbolea nchini hasa mkoani Ruvuma, Waziri Bashe alisema bei za mbolea duniani zimekuwa zikiongezeka kutokana na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji na mahitaji hususan kwenye nchi zenye watumiaji wakubwa wa mbolea kama vile China na India.

Alisema ongezeko hilo kwa msimu wa 2021/2022 limechangiwa na athari za UVIKO- 19 na vita kati ya nchi ya Russia na Ukraine ambao ni wazalishaji wa malighafi zinazotumika katika utengenezaji wa mbolea.

Aidha alisema Mwezi Machi, 2022 kupitia TFRA imetoa bei elekezi za mbolea za DAP, UREA, CAN na SA kwa Mikoa mbalimbali nchini ikiwemo Mkoa wa Ruvuma.

Pia alisema katika kuondokana na utegemezi wa uagizaji wa mbolea nje ya nchi, serikali inaendelela kuvutia uwekaji wa viwanda vya mbolea hapa nchini ili kupunguza gharama za mbolea kwa mkulima.

Aliwasisitiza viongozi wa Mikoa na Wilaya kuhakikisha kuwa bei elekezi zilizotolewa zinazingatiwa katika vituo vyote vya mauzo ya mbolea.



Ukurasa 12

**Alidumisha staili chama kinabuni, kishindo cha utekelezaji serikalini**



Ukurasa 13

Rais Samia katika orodha ya kinamama maarufu duniani

# siasa





Ukurasa 14

**ANITA AMONG**

**Mwanamama aweka rekodi mpya ya uspika Uganda**

MIAKA 100 YA MWALIMU NYERERE




Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia kwenye mdahalo wa miaka 100 ya Baba wa Taifa. **PICHA: MTANDAO**

# Rais Samia ashuku kulegezwa misingi ya Baba Taifa, akumbusha ishikiliwe

KAMA Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere angekuwa hai, leo Aprili 13 angekuwa anasherehekea kutimiza miaka 100 ya kuzaliwa. Lakini, ni bahati mbaya ameshatangulia mbele ya haki.

Wiki iliyopita, Rais Samia alishiriki kwenye mdahalo wa kitaifa wa kuadhimisha miaka 100 ya kuzaliwa Baba wa Taifa uliofanyika katika Shule ya Uongozi, Kibaha mkoani Pwani, akigusia namna jamii inapotosha baadhi ya maeneo yanayobeba ujumbe.

Rais anasema, Mwalimu Nyerere alilijenga taifa lenye umoja na mshikamano alipinga ubaguzi hata udini, ukanda na ukabila, hivyo ni wajibu wa Watanzania kupinga vitu hivyo ikiwa ni sehemu ya kumuenzi.

Anafafanua, baadaye watu wakaanza kujuana kwa rangi, udini, kabila, ukanda na itikadi, hivyo kuna kazi ya kuirudia zama Tanzania kuwa moja, baada ya kutetereka.

"Hapa kuna kazi ya kufanya kidogo na panaumiza kichwa kidogo," Rais Samia, anasema.

**NYENZO UMOJA**

Msisitizo wake Rais Samia ni kwa Watanzania kurejea umoja wao waliotengenezewa na Baba wa Taifa, aliyefanya kazi hiyo, huku akihimiza matumizi ya lugha Kiswahili kabla na baada ya uhuru kama nyenzo ya kujenga umoja huo wa kitaifa.

"Hayati Baba wa Taifa amewaachia somo kubwa Watanzania la kuwa wazalendo kwa taifa kwa kuwa alilipenda na kujitoa mhanga kwa ajili ya Watanzania," anafafanua.

Anasema, mwasisi huyo wa taifa aliwafundisha Watanzania somo kubwa la uzalendo kitaifa na binafsi akauonyesha uzalendo usio na shaka, akilipenda taifa na alikuwa tayari kujitoa mhanga kwa ajili ya Watanzania.

"Uzalendo wake ulijionyesha wakati wa kupigania uhuru alipoacha kazi ya ualimu na kujikita katika kulikomboa taifa na wenzake na akapitia magumu na changamoto nyingi kwa ajili ya kulikomboa taifa hili," anasema.

Anaongeza kwamba aliwezesha lugha ya Kiswahili kukubalika na Waafrika na sasa ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Utamaduni (UNESCO) kuitengea siku yake maalumu.

**ANAFUATA NYAYO**

Tangu baada ya kula kiapo kuongoza nchi Machi 19 mwaka jana, Rais Samia anahimiza suala la Watanzania kuwa wamoja kitaifa na kuacha tofauti zao, washikamane kwa ajili ya maendeleo yao, pasipo kujali itikadi za vyama, dini kabila na kila aina inayoweza kuwatenganisha Watanzania. Lile lililosisitizwa na Baba wa Taifa, hata wakafuata marais wengine na sasa analiendeleza.

Rais Samia ananadi imani yake kwamba Tanzania itajengwa na umma wa vyama mbalimbali vya siasa, kabila na dini tofauti kuumba umoja huo na si kujenga mgawo kiitikadi na hisia zingine.

Hivi karibuni akifungua mkutano wa kitaifa wa haki, amani na maridhiano, Rais amerudia kusema Tanzania haitajengwa na ama chama au mtu mmoja, hivyo kunahitajika kuwapo ushirikiano.

Anahimiza viongozi mbalimbali nchini kuwa watumishi wa watu na kwamba mawaziri na watendaji wengine wa serikali, wafanye kazi kwa kuwa wanapimwa kwa utendaji wao.

Katika hilo amekiagiza Chuo cha Taifa cha Siasa, Uongozi na Maadili cha Mwalimu Nyerere, Kibaha kujikita kuwa kituo cha kuhifadhi kumbukumbu za historia za waasisi zitatumika kufundisha na kuongoza nchi kwenye mambo mbalimbali, kwa kuwa kufanya hivyo utakuwa ni mwendelezo wa kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa uongozi wake uliotukuka.

HATUA ZA KUSHIKA HATAMU

# Alidumisha staili chama kinabuni, kishindo cha utekelezaji serikalini

• Mapinduzi makubwa yakashuhudiwa

**Na Peter Orwa**

LEO hasa ndio kunashuhudiwa miaka 100 ya kuzaliwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliyetangulia mbele za haki miaka 22 na nusu iliyopita.

Nyerere akijumuishwa kwa yote, ana uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya kila Mtanzania hadi sasa. Hapo inaweza kutolewa ushahidi wa alichotamka Rais Samia Suluhu Hassan, mwishoni mwa wiki akisema Mwalimu Nyerere amebaki marejeo makuu kwa mambo mbalimbali yanayoamuliwa katika awamu tofauti za kiserikali hadi sasa.

Ikianzia kisiasa, mwangaza aliodumu nao ni wa chama kushika hatamu za uongozi kitaifa, kuanzia TANU na baadaye kuzaliwa CCM, miaka 45 iliyopita.

Fikra na mwelekeo ilianzia ndani ya nyumba ya chama na kisha maagizo ya utekelezaji ndio yakahamia kwenye serikali, huku chama kikibeba dhamana ya kuiwajibisha mamlaka hiyo ya kidola.

Ni aina ya itikadi inayojitokeza sana hata ndani ya uongozi wa CCM hivi sasa, kwa ushuhuda Katibu Mkuu mpya wake, Daniel Chongolo alipojiunga muda mfupi wa uongozi wake, amekuwa akizunguka nchini kukagua ufanisi wa miradi ya serikali, kama inaendana na ilani waliyopewa.

Ni staili inayotumika kuainisha ahadi zilizoko kwenye ilani yake na nyinginezo kupata picha halisi na ufafanuzi, iwe mafanikio au kusuasua.

Siku chache zilizopita, akifunga kikao cha Mkutano Mkuu wa CCM, Makamu Mwenyekiti (Bara), Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, ameahidi ndani ya muda mfupi ujao, chama kitawaita mawaziri wake kujadiliana nao kwa kina hatua za kukidhi mahitaji ya umma na maendeleo yake.

### HATUA ZA KIHISTORIA

Ni miaka yote tangu kupatikana uhuru wa Tanganyika, Rais Nyerere alizamisha mtazamo huo kuona kunakuwapo chama imara - TANU, kinashika dhamana za uongozi wa Tanganyika zama hizo na ndio maana kwa muda akaweka kando cheo chake, waziri mkuu wakati huo, ili akaimarishe chama, akijua deni lililofuata chama kitakaposhika hatamu kamili za uongozi.

Hata ilipofika mwaka 1964 fikra zilizojengwa kutoka ndani ya vyama TANU na ASP, ndio zikaibua wazo la muungano wa Tanganyika na Zanzibar, hata likatimia.

Haukupishana muda mrefu katika mwaka huo, pia itikadi ya chama ikadumishwa rasmi, maisha na maendeleo ya umma kitaifa ikasimama rasmi katika falsafa ya Ujamaa na Kijitegemea.

Chama cha TANU chini ya uenyekiti wa Nyerere, kikatangaza falsafa rasmi ya chama hicho kwa Ujamaa. Tangu wakati huo, maisha ya kawaida ya umma na utendaji kiserikali, yakajikita katika itikadi hiyo.



Mwalimu Julius Nyerere, alipokuwa na timu yake kwenye nyendo za kampeni ya uchaguzi wa Tanganyika. **PICHA: MTANDAO**

> Oktoba 10, 1953 Mwalimu Nyerere, Abdulwahid Sykes, Ally Sykes, Dossa Aziz na John Rupia walikutana kujadili namna ya kuibadili TAA kuwa chama kamili cha siasa.

Ukawa muda wa kutekeleza falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea, pakashuhudiwa hata ndani ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kukaundwa rasmi Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), ambako vijana walipelekwa mafunzoni na kuzalisha mali, kwa mujibu wa sheria na wapo wanaojitolea.

Ni zama ambazo pia mafunzo ya mgambo yakapamba moto, kila raia kuwa mlinzi wa taifa, umma vijijini na sehemu za kazi walishiriki vyema na msaada wao ukaonekana katika vita ya Tanzania na Uganda na hadi sasa jeshi hilo lina uhai.

Hadi kufika mwaka 1967, wakati serikali ikiwajibika kutekeleza na kupanga mipango iliyoasisiwa mwaka 1964, kupitia Azimio la Arusha, ikitafasiri namna serikali itamiliki njia kuu za uchumi, kwa nyendo za kijamaa; watu kufanya kazi pamoja kwa faida ya wote.

Utekelezaji wake kiserikali ndio kulikoshudiwa mengi ya utafishwaji mali binafsi na kuundwa mifumo mipya ya kitaasisi serikalini kukidhi mahitaji hayo.

Mwaka 1971, kukiwa kumeshuhudiwa mapinduzi makubwa katika mifumo ya uzalishaji kitaifa, viwanda vingi kujengwa na kuwapo wafanyakazi wengi kitaifa, chama TANU kikapitisha Mwongozo wa kuanzishwa Mabaraza ya Wafanyakazi, ikiwa sehemu ya kutekeleza yatokanayo na Azimio la Arusha. Leo hii ni sehemu ya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini.

Mwaka 1972, chama cha TANU kikaona haja ya serikali kuimarisha mikakati ya kuimarisha mahitaji ya wakulima na sekta hiyo kwa taifa, kukapitisha Azimio la Musoma lililojikita katika mambo mbalimbali ya maendeleo shambani, uvuvi na ufugaji.

Penye utekelezji wake ndiko kukashudiwa mikakati na dhana 'Kilimo ni Uti wa Mgongo' serikali ikieneza mengi ya kujenga sekta kuanzia maofisa ugani, vijijini na mbolea, maofisa uvuvi na wanaohusika na ufugaji mbalimbali.

Ndani ya miaka miwili kukaenezwa namna bora ya mifumo wa kuishi pamoja kupitia vijiji vya kawaida na vya ujamaa, umma ukiwa na maisha ya pamoja, ikiashiria mawili kwa wakati mmoja, itikadi ya kijamaa na muundo wa kimaendeleo.

Vivyo hivyo, ndivyo tena mwaka 1974, TANU ikapitishwa Azimio la Musoma ambalo lilikazia elimu, kuzama zaidi katika elimu ya msingi, pia kuwezesha umma wa Watanzania ambao hawakupata fursa kujua kusoma na kuandika.

Mwaka huohuo, TANU pia ilipitisha Azimio kuhusu Ukombozi wa Afrika, kuimarisha uwajibikaji ulioanza kimataifa kukomboa nchi nyingine zilizo chini ya mkoloni Afrika.

Tanzania ilikuwa mwenyeji wa wanaopigania juhudi hizo, Mfano wa mafanikio ni uhuru wa Msumbiji uliopatikana miaka miwili baadaye, 1976 hata kufanyika sherehe kubwa kwenye Uwanja wa Taifa (sasa Uwanja Uhuru), jijini Dar es Salaam.

Siku zote, mzizi wa uamuzi mkuu kitaifa ilianzia kwenye chama, utekelezaji wenye vishindo ukihamia serikalini na chama kikabaki msimamizi kama afanyacho Chongolo sasa.

### ALIKOTOKEA NYERERE

Mwaka 1929, TAA iliundwa ikiwa na wajumbe: Kleist, Mzee Bin Sudi, Ibrahim Hamis, Zibe Kidasi, Ali Said Mpima, Suleiman Majisu, Raikes Kusi, Rawson Watts na Cecil Matola

Mwaka 1950, TAA iliwasiliana na wenzao wa KAU (Kenya African Union) nchini Kenya kupata ujuzi zaidi. Abdulwahid alitumwa Nairobi, akakutana na Mwenyekiti Jomo Kenyatta, kujenga mawasiliano kati yao.

Mwaka 1951, kukaundwa tawi la siasa la chama TAA likiwa na wajumbe wafuatao: Abdulwahid Sykes (Katibu), Sheikh Hassan bin Amir, Hamza Kibwana Mwapachu, Said Chaurembo, Dk. Kyaruzi, John Rupia na Stephen Mhando.

Mwaka huo, Kenyatta akakutana tena na viongozi wa TAA mjini Arusha na wajumbe wa TAA walikuwa: Abdulwahid Kleist Sykes, Dossa Aziz na Stephen Mhando.

Mwaka 1952, Abdulwahid alichaguliwa Rais wa TAA na ndio mdau mpya wa Mwalimu Nyerere akatambulishwa kwa Abdulwahid na Kasela Bantu. Ikawa kila Jumamosi, Mwalimu Nyerere akawa anakutana na kina Dossa Azizi, Ally Sykes, Abdulwahid Sykes, Dustan Omar na Mhando kujadili mustakbali wa nchi ya Tanganyika, wakikusanyika nyumbani kwa Dossa Azizi Mtaa wa Congo au Mtaa wa Stanley, nyumbani kwa Abdulwahid.

Dossa Azizi ndiye mara nyingi alimrudisha Mwalimu Nyerere kwa gari lake Pugu anakoishi (St. Francis College) baada ya mkutano.

Mwaka 1953, Nyerere akachaguliwa kuwa Rais wa TAA. Wazee walimpa nguvu ya kisiasa mara baada ya kujiunga nao. Hao ni wazee: Sheikh Hassan bin Amir, Sheikh Suleiman Takadir, Mzee Mohammed Jumbe Tambaza, Mshume Kiyate na Mwinjuma Mwinyikambi. Wengine walikuwa Rajab Diwani, Makisi Mbwana, Sheikh Haidar Mwinyimvua na Idd Faiz Mafongo. Aidha walikuwepo Idd Tosiri, Sheikh Mohamed Ramia na Mashado Ramadhani Plantan.

Oktoba 10, 1953 Mwalimu Nyerere, Abdulwahid Sykes, Ally Sykes, Dossa Aziz na John Rupia walikutana kujadili namna ya kuibadili TAA kuwa chama kamili cha siasa.

1954: TANU ikaanzishwa na wajumbe wa mkutano uliojadili kuibadili katiba ya TAA kuwa TANU, walikuwa Abdulwahid Sykes, Julius Nyerere, Tewa Said Tewa, Dossa Aziz, Ally Sykes, Kasela Bantu, , Abubakar Ilanga na Saadan Abdu Kandoro.

Wengine walikuwa S.M. Kitwana, C.O. Milinga, Patrick Kunambi, Gerimano Pacha, Japhet Kirilo na L.M. Makaranga, Joseph Kimalando na John Rupia.

Julius Nyerere alipewa kadi ya TANU namba moja. Kadi namba mbili ikaenda kwa Ally Sykes na Abdulwahid akachukua kadi namba tatu, Dossa Azizi nne, kadi namba tano akapewa Phombeah, sita ni Dome Okochi, saba John Rupia, Bibi Titi Mohamed kadi namba 16 na Idd Tosiri, namba 25.

# Rais Samia katika orodha ya kinamama maarufu duniani

Na Christina Mwakangale

**• Kwenye majina 100 ametinga • Wanatajwa ushawishi wao juu**

UNAPOZUNGUMZIA wanawake maarufu duniani, yumo Samia Suluhu Hassan, mkuu wa Tanzania, kati ya kinamama wachache waliowahi kushika wadhifa huo hata barani Afrika.

Jarida maarufu la Forbes, 'The World's 100 Most Powerful Women' lilimuweka Rais Samia yumo kwenye orodha ya wanawake 100 maarufu.

Kati ya hao wenye asili ya kiafrika na kushiriki nyadhifa za juu yumo Makamu wa Rais Marekani, Kamala Harris na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Biashara Duniani (WTO), Ngozi Okonjo-Iweala.

Kwenye jarida hilo la 18 la mwisho wa mwaka uliopita, lina orodha inayobainisha viongozi wenye nguvu duniani wakiwamo wakurugenzi wakuu na wajasiriamali mashuhuri, wakuu wa nchi, wahisani waanzilishi na watungasera ambao wanatatua matatizo ya kijamii.

Katika orodha ya viongozi hao wanawake 100, wamo wakurugenzi wakuu wa taasisi na mashirika wapatao 40, pamoja na marais wanawake wachache wakitajwa wawili, akiwamo rais Samia na rais Zuzana Ǎputová wa Slovakia.

Pia, wanawake hao wa nguvu 2021 wana ushawishi mkubwa katika kutoa mapato kutokana na shughuli tofauti yanayokadiriwa kufikia dola trilioni 3.3 na kutoa ajira kwa wafanyakazi milioni 6.7.

Kadhalika orodha ya wanawake hao inahusisha waliomo kwenye viwango vya mabilionea duniani walio na thamani za mali ya dola bilioni 167.

Jarida hilo la Forbes, linamuelezea Rais Samia kwamba alikuwa mwanamke wa tano mwanamke kutoka barani Afrika kulihutubia Baraza la Umoja wa Mataifa.

Rais Samia kwa kipindi cha miezi tisa madarakani yapo aliyotazama kwa ukaribu hususan kijinsia ikiwamo kufanikisha elimu ya juu na kuwafikia wote, kwa kutenga Sh. Bil 70 zaidi ya zilizotengwa ambazo ni bilioni 500, kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mkopo kwa ajili ya elimu ya juu.

Rais Samia, ametangaza kuwaruhusu wanafunzi waliokatiza masomo yao kwa kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata mimba kurejea masomoni.

Pia, rais ameongeza vyumba vya madarasa na zimetengwa Sh. Bilioni 125 kwa ajili ya kukamilisha maboma 10,000.



Juu kushoto, anaanza Mackenzie Scott, katikati Rosalind Brewer na Reese Witherspoon, Mstari wa chini kuanzia kushoto, Samia Suluhu Hassan, Laura Cha na Kamala Harris. Chini; Rais Samia akiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**



### WENGINE DUNIANI

Makamu wa Rais Marekani, Harris Kamala, Januari mwaka huu ameingia katika orodha ya kuwa mwanamke wa kwanza mweusi, mwenye asili ya Marekani na Asia, kushika wadhifa huo.

Mwaka 2016, Harris, alikuwa mwanamke wa kwanza kuchaguliwa kuwa mmoja wa maseneta, Marekani, huku mwaka 2010, Harris akiwa pia mwanamke wa kwanza mwenye asili hiyo, kuhudumu kama Mwanasheria Mkuu California.

Harris, ni mkimbizi aliyezaliwa Oakland, walikoishi wazazi wake wakimbizi huku mama yake akiwa ,mhindi na babake raia wa Jamaica.

Pia Harris, ni mhitimu wa Chuo cha Howard University alumna, chenye historia ya zamani kama chuo kilicho maalum kwa watu weusi,

### TSAI

Rais wa Taiwan, Tsai Ing-wen, anayeungwa mkono na chama ambacho kina historia ya kuipinga China, alitawazwa mwaka 2016, kushika mamlaka hayo.

Tsai, ni mwanamke wa kwanza kuwa Rais wa Taiwan, yumo kwenye orodha hiyo, wanawake wa nguvu duniani.

Hata hivyo, msomi huyo wa sheria mwenye umri wa miaka 59, alipuuza onyo lililotolewa wakati fulani na China kumtaka akubali kufanya mazungumzo, kutambua kuwa Taiwan na China ni taifa moja.

### OPRAH

Mtangazaji huyo mashuhuri duniani, Oprah Winfrey naye ameorodheshwa kwenye jarida hili la wanawake wa nguvu 100 mwaka huu, ambaye anaendesha kipindi cha televisheni kwa takribani miaka 25 sasa, na kubadili media kuwa sehemu ya biashara.

Kipindi chake kinakadiriwa kumuingizia kiasi cha dola bilioni mbili. Mwaka 2011, Winfrey alizindua chaneli yake ya OWN, huku asilimia 25.5 ya thamani ya mtandao wa chaneli hiyo ikifikia thamani ya dola milioni 65.

> Jarida hilo la Forbes, linamuelezea Rais Samia kwamba alikuwa mwanamke wa tano mwanamke kutoka barani Afrika kulihutubia Baraza la Umoja wa Mataifa.

### APUTOVÁ

Rais Zuzana Ǎputová wa Slovakia, mpinga rushwa, mwanaharakati wa mazingira na mwanasheria, yumo kwenye orodha hiyo, akiwa mamlakani kwa kipindi cha miaka mitano baada ya kuingia madarakani Juni 2019.

Kwa umri wake wa miaka 47 nchini Slovakia, ni kijana mwenye umri huo kushika wadhifa huo katika umri mdogo lakini hata kidunia ni rais mwanamke aliyeingia madarakani katika umri mdogo. Katika hotuba yake wakati akila kiapo, Caputova alitoa matumaini kwa watu wake kwamba ataboresha muhimili wa kisheria na kupambana na rushwa akipewa jina la 'sauti pekee ya kisiasa katika lindi la bahari ya unyanyasaji.''

Umaarufu wake ulianza baada ya muongo mmoja wa mapambano dhidi ya dampo lenye sumu katika mji wake wa Pezinok, na harakati hizo kumfanya apokee tuzo mwaka 2016 ua 'Goldman Environmental Prize'.

Aputová alishinda uraisi mwaka 2019 kwa asilimia 58 ya kura zote, akiahidi kuimarisha mahusiano na nchi jirani.

### SERENA

Mwanamichezo huyo maarufu kwenye tenisi takribani miaka 20, Serena Williams, ni mwanamke anayeingia kwenye orodha hii, ana ushirika kwenye kampuni mbalimbali zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 94. Utajiri wake zaidi ukitokana na kipaji chake katika mchezo huo.

Pia, orodha hiyo ina wanawake wenye asili ya Kiafrika wakiwamo waimbaji mashuhuri Rihanna, Beyonce, ambao wanatajwa katika umaarufu wa kifedha kutokana na vipaji vyao.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Mwanamama aweka rekodi mpya ya uspika Uganda

Na Christina Mwakangale

ANITA Among ndiye Spika wa Bunge la Uganda, kwa sasa akichukua nafasi ya mtangulizi wake Jacob Oulanyah, ambaye amefariki dunia wiki chache zilizopita akipatiwa matibabu, huko Marekani.

Taarifa zinaeleza kwamba Oulanyah alikuwa akipatiwa matibabu katika moja ya hospitali zilizopo Seattle, jijini Washington.

Among (48), Mbunge wa Jimbo la Bukedea aliibuka na ushindi baada ya kupata kura 401 za wabunge huku mpinzani wake Mbunge wa Manispaa ya Bugiri, Asuman Basalirwa, akiambulia kura 66.

Inaelezwa ushindi wa Among umechangiwa pakubwa na chama cha NRM, chenye idadi kubwa ya wabunge bungeni huku Basalirwa anayetokea upinzani akiwa na idadi ndogo. NRM ina wabunge 330 kati ya 519 ya wabunge wa kuchaguliwa.

"Kwa neema za Mungu, tutafanya juhudi kulifanya taifa letu kuwa sehemu nzuri kwa wote, kwa heshima ya kuendeleza alichokiacha kiongozi na kaka yetu Jacob Oulanyah," anasema Among, mara tu baada ya kuibuka mshindi na kutangazwa na Jaji Mkuu Alphonse Owiny Dollo.

Rais Yoweri Museveni alitangaza kifo cha Spika wa Bunge la Uganda kwenye akaunti yake ya Twitter, Jumapili, wiki iliyopita katika ujumbe wake, rais alimtaja kiongozi huyo kama kada mzuri.

Ingawa kilichosababisha kifo cha Oulanyah hakijabainishwa, alilazwa hospitali nchini Marekani kwa zaidi ya mwezi mmoja.

Raia wengi wa Uganda walikuwa wamemtabiria Among kushinda kutokana na chama chake cha NRM kuwa na idadi kubwa ya wabunge ambao ni zaidi ya asilimia 80 katika bunge hilo.

Hata upinzani nao unatajwa walifahamu kuwa ingekuwa vigumu kumshinda mgombea wa chama tawala, sababu kuu, idadi yao.

Mara tu baada ya kutangazwa mshindi, Anita Among aliapishwa kuendesha shughuli za bunge akikabidhiwa wadhifa huo na Rais Museveni pamoja na Jaji Mkuu Dolo.

Hii ni mara ya pili kwa mwanamke kuweka historia ya kushikilia wadhifa huo wa spika la bunge, Uganda.

Rebecca Alitwala Kadaga, ndiye alikuwa wa kwanza kushikilia wadhifa huo akiwa spika kwa kipindi cha miaka 10.

Hata hivyo alishindwa katika kutetea kiti hicho, wakati chama tawala NRM kilipomteua naibu wake Jacob Oulanya.

Kifo cha Oulanya aidha kimeshuhudiwa kuibua mabishano ya kikabila pale Jaji Dollo alipowashutumu watu aliodai ni wa jamii ya Baganda kwa kufanya maandamano nchini Marekani wakipinga kupelekwa kwa Oulanya huko kwa matibabu.

Kusafirishwa kwake hadi Marekani kwa matibabu kulizua mjadala miongoni mwa Waganda, ambao walidai kuwa iligharimu pesa nyingi sana za walipakodi.

Oulanyah alichukua hatamu ya uongozi wa bunge la Uganda Mei mwaka jana. Alikuwa naibu spika kuanzia mwaka 2011.

Alikuwa na sifa ya kuanzisha vikao vya bunge kwa wakati na kila mara alitoa wito kwa wabunge kuimarisha ubora wa mijadala, kwa kujadili mambo yaliyo na ufahamu wa kina.

Ni mwanasheria na mwanasiasa wa muda mrefu. Aliwahi kuwa mbunge wa Bunge la Kaunti ya Omoro, Kaskazini mwa nchi.

Oulanyah alikuwa miongoni mwa wanasiasa kutoka eneo hilo walioshiriki katika mazungumzo ya amani kati ya serikali ya Uganda na waasi wa Lord's Resistance Army (LRA), walioongozwa na Joseph Kony, miaka ya 2000.



Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson (wa pili kulia) akishiriki shughuli za mazishi ya aliyekuwa Spika wa Bunge la Uganda, Jacob Oulanyah, yaliyofanyika nchini Uganda hivi karibuni na kushirikisha wajumbe wa nchi mbalimbali. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> "Oulanyah alichukua hatamu ya uongozi wa bunge la Uganda Mei mwaka jana. Alikuwa naibu spika kuanzia mwaka 2011.



Spika wa sasa nchini Uganda, Anita Among.

### AMONG NI NANI

Among alizaliwa Wilaya ya Bukedea, Novemba 23 mwaka 1973. Alipata elimu ya msingi na sekondari kwenye shule za umma. Ana shahada ya Usimamizi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu, Makerere , mwaka 2005.

Mwaka 2008, alitunukiwa shahada ya pili katika fani hiyo hiyo pia chuoni Makerere.

Kadhalika, mwaka 2018, Among alihitimu katika Chuo Kikuu cha Kimataifa Kampala (KIU) shahada ya sheria.

Mwaka 1998 hadi 2006, Among alifanya kazi benki ya Centenary, moja kati ya benki kubwa Uganda ,hadi anaondoka alikuwa katika ngazi ya meneja wa tawi.

Pia amewahi kuhudumia kama mhadhiri wa chuoni KIU.

Among, alikuwa mwanachama kutoka upinzani kwa muda mrefu kutoka chama cha Democratic Change , mwaka 2016 aliwania kiti Cha ubunge kama mgombea binafsi na kushinda.

Mwaka juzi, alijiunga na NRM baada ya kuporomoka kwa chama chake cha FDC.

Among, amechaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Uganda, Machi 25, mwaka huu, akichukua nafasi ya Oulanyah, aliyefariki siku chache akitibiwa Marekani.

• ***Kwa msaada wa taarifa kimataifa.***





# Wajasiriamali washauriwa kujiepusha mikopo umiza

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAJASIRIAMALI wameshauriwa kukopa kwenye taasisi za kibenki ili kujiepusha na mikopo inayotolewa mitaani kwa riba kubwa ambayo imekuwa ikichangia kuua mitaji yao.

Meneja wa mkoa wa Dodoma Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Mohammed Masud Khamis, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wafanyabishara ndogo ndogo wa Mkoa wa Dodoma.

Alisema wajasiriamali wanapaswa kukopa kwenye benki ambazo tozo ya riba zao ni nafuu kwa ajili ya kukuza biashara,tofauti na zinazotozwa na taasisi za kifedha za mitaani.

Meneja alisema kuwa taasisi fedha za mitaani zimekuwa na riba inayoumiza ambayo inasababisha wajasiriamali kufilisika na kuiua mitaji yao.

"Nitoe rai kwa wafanyabishara wadogo, wajielekeze kukopa mikopo yao kwenye taasisi za kifedha za serikali ili waepukane na balaa la kufilisiwa mali zao na kufilisika kifedha, kwetu sisi Benki ya Watu wa Zanzibar hutoa huduma zake kwa gharama nafuu kwa wafanyabishara wote wakubwa kwa wadogo na tupo zaidi ya miaka 56 tukitoa huduma ya kifedha na tozo yetu ni ndogo,"alisema.

Aidha alishauri fedha wanazozikopa zitumiwe kwa malengo mahususi,badala ya kuzielekeza kwenye starehe za anasa zisizo kuwa na tija.

Awali, baadhi ya wafanyabiashara ndogo ndogo wa Soko Kuu la Majengo, waliziomba taasisi za kibenki kutochelewesha mikopo yao pale inapotokea mwombaji ametimiza vigezo vya kupatiwa mkopo.

Hamisi Hussen alisema kuwa wafanyabiashara wamejikuta wakikimbilia taasisi za mitaani za kifedha kutokana na uharakishaji wa fedha wanazozitoa pamoja na kuwa zinatolewa kwa riba kubwa.

**Aidha alishauri fedha wanazozikopa zitumiwe kwa malengo mahususi,badala ya kuzielekeza kwenye starehe za anasa zisizo kuwa na tija.**

# Kima cha chini cha mshahara sekta binafsi kufanyiwa utafiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, amezindua Bodi ya Mishahara kwa sekta binafsi, huku akiitaka kufanya utafiti na kutoa mapendekezo ya kima cha chini ya mshahara kwa sekta hiyo.

Kima hicho kitazingatia sheria, kanuni na taratibu zilizopo. Akizindua bodi hiyo jana, Prof. Ndalichako alisema kwa muda mrefu bodi hiyo haijakaa na watanzania wamekuwa wakisubiri kuona kazi yake.

Alisema bodi ina jukumu la kufanya utafiti, uchunguzi na kutoa ushauri kwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya kazi kuhusu kima cha chini cha mshahara kisekta.

"Mei mosi mwaka 2021 Mheshimiwa Rais Samia alizungumzia bodi ya mishahara haijakaa kwa muda mrefu nimeona ni jambo ambalo tulisukume ikiwa ni utekelezaji wa matakwa ya kisheria lakini utekelezaji wa maelekezo ya Rais."

"Ni jukumu lenu kufanya utafiti na kutoa mapendekezo kwangu kuhusu kima cha chini cha mshahara katika sekta binafsi, na mtatoa mapendekezo kisekta na katika kutekeleza majukumu haya, bodi ina jukumu la kuzingatia maslahi ya nchi na hali ya uchumi, uwezo wa watu kulipa mshahara, mnaangalia hali ya mfanyakazi kumudu maisha mnaangalia pande zote,"alisema.

Alibainisha kuwa muundo wa bodi hiyo una uwakilishi wa utatu ambao ni serikali, waajiri na wafanyakazi.

"Ni matumaini yangu kuwa mtafanikisha utekelezaji kwa kuzingatia kanuni, majadiliano kwa kuwa suala la kufikia kiwango cha mshahara linahitaji majadiliano,pia mzingatie matakwa ya sheria ya kazi na mikataba ya kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (ILO),"alisema.

Alisema mapendekezo ya mishahara hayatolewi kwa kukaa mezani lazima kufanya utafiti ili kuzingatia vigezo vilivyowekwa.

"Kima cha chini cha mshahara ni suala muhimu sana ambalo linapaswa kushughulikiwa kwa umakini kama nilivyosema inapaswa kuangalia hali ya uchumi, pia maisha na maslahi ya wafanyakazi wanaoishi dunia ya sasa iliyokumbwa na changamoto za Uviko-19, vita ya Urusi na Ukraine kwa hiyo kuna vitu vingi vimeharibika ambavyo vinamuathiri mfanyakazi,"alisema.

Prof. Ndalichako alisema Rais Samia amedhamiria kujenga utumishi wa moyo ili mtumishi aone fahari kutekeleza majukumu yake.

Aliitaka bodi kutoa mapendekezo ambayo yataamsha ari ya kufanya kazi kwa watumishi.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Jamal Katundu, alisema wajumbe wa bodi hiyo wataandaa mpango kazi wao kwa kushirikiana na wataalamu ambao utaonesha majukumu watakayoyafanya na lini watatoa mapendekezo ya kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Suleiman Ahmad Rashid, aliahidi bodi kufanya kazi kwa umakini na kuzingatia sheria, taratibu ili lengo linalokusudiwa lifikiwe.

"Ushauri mzuri tutakaoutoa utapatikana baada ya sisi wenyewe kufanya utafiti, tutateua watu wafanye utafiti na tutaangalia na baada ya kuridhika nazo tutakushauri ili utekelezaji wake ulete morali katika nchi yetu," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga (kulia), akimsikiliza Meneja Mkuu wa OreCorp Tanzania, Damien Valente (kushoto), wakati wa makabidhiano ya msaada wa spika na kipaza sauti yenye lengo la kuunga mkono programu ya kupambana na UVIKO-19 na kampeni ya elimu ya chanjo wilayani humo, mkoani Mwanza juzi. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Binuru Shekidele. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU, ZAECA zaagizwa vita dhidi ya rushwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kushirikiana na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) katika mapambano dhidi ya rushwa ili kujenga taifa lenye maadili.

Mhagama alitoa maelekezo hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa TAKUKURU na ujumbe kutoka Mamlaka ya ZAECA ulipomtembelea ofisini kwake kujitambulisha.

Alisema ushirikiano anaoutaka uwe umejikita katika kujenga na kuimarisha utendaji kazi wa TAKUKURU na ZAECA ili kuwa na mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya rushwa.

"Ninaomba ushirikiano huo ujikite zaidi katika kubadilishana uzoefu kwenye uchunguzi wa vitendo vya rushwa, uendeshaji wa mashtaka na kuzuia vitendo vya rushwa," alisisitiza.

Alisema ushirikiano katika kupambana na rushwa hauepukiki kwa kuwa tatizo la vitendo vya rushwa ni suala mtambuka ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania licha ya utofauti wa sheria zinazoongoza taasisi hizi mbili za TAKUKURU na ZAECA katika mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema kuna ulazima wa kuwa na mbinu na mikakati ya pamoja itakayoliwezesha taifa kupambana na vitendo vya rushwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA, Kamishna wa Polisi, Ahmed Makarani, alisema amepokea maelekezo hayo na kuahidi kuzingatia katika utendaji kazi wao wa kila siku ili kufanikiwa katika mapambano dhidi ya rushwa.





# DC ataka sheria kuwabana wazazi kuchangia chakula

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune ameliomba baraza la madiwani kuharakisha mchakato wa kutunga sheria ndogo itakayowabana wazazi na walezi kuchangia chakula shuleni kwa lengo la kupunguza utoro na kuongeza ufaulu.

Mfune alitoa rai hiyo jana wakati wa kilele cha Wiki ya Elimu wilayani hapa ambayo ilifanyika katika viwanja ya Shule ya Sekondari Rujewa na kuhudhuriwa na wanafunzi kutoka shule za msingi na sekondari, walimu, wakuu wa idara na wadau wa elimu Mbarali.

Alisema utaratibu wa watoto kupatiwa chakula shuleni utaleta tija kwa wanafunzi kwa kuwa badala ya kutoroka kufuata chakula nyumbani watabaki kuendelea na masomo kwa vile chakula kitapatikana.

"Ni wakati sasa baraza la madiwani kupitisha haraka sheria ndogo ya kuwabana wazazi kuchangia chakula shuleni. Tunafanya hivyo baada ya kubaini ukosefu wa chakula ni moja ya sababu zinazochangia watoto kutokufanya vizuri shuleni. Sasa ni wakati wa kukamilisha mchakato huo na sheria ianze kutekelezwa mara moja," alisema Mfune.

Katika kuadhimisha wiki ya elimu ambayo hadi sasa ni miaka minne imefika tangu kuanzishwa kwake, Mfune alisema yanatoa nafasi kwa walimu na wanafunzi kujitathmini mambo ya kuyafanya ili kufanya vizuri katika mitihani.

Licha ya kueleza mikakati ya kuinua ufaulu wilayani Mbarali, aliwapongeza wanafunzi wote walioonyesha ubunifu wao kwa kutumia teknolojia mbalimbali wakati wa maadhimisho hayo. Alisema ubunifu huo una tija kwa wanafunzi kwa sababu wameweza kuonyesha vipaji walivyo navyo ili kusaidiwa na walimu, serikali na wadau mbalimbali.

Alisema lengo la Wiki ya Elimu ni kuibua vipaji vya watoto na kuviendeleza, kukuza ubunifu miongoni mwa wanafunzi katika nyanja za ugunduzi wa teknolojia mpya, kuwajengea uwezo wa kuzungumza mbele ya hadhira nje na ndani ya mazingira waliyoyazoea.

Kutokana na utaratibu huo, alisema wilaya imefika wastani wa ufaulu wa mitihani kutoka asilimia 80 hadi 93 na kwamba hawajaridhika na kiwango hicho, hivyo wanaendelea kupambana ili kuhakikisha Mbarali inakuwa kinara kwenye matokeo ya mitihani kuanzia mkoa hadi taifa.

Aliwataka walimu kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza ufaulu na wanafunzi kuzingatia yale wanayofundishwa na kusoma kwa malengo ili waweze kutimiza ndoto zao.

Mfune alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuipatia wilaya fedha kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa, samani na matundu ya vyoo.

Katika taarifa yake, Ofisa Elimu Sekondari, Anna Shitindi, alisema katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2022 wamedahili wanafunzi 16, 552 kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza.

Alitaja mafanikio mengine kwenye Idara ya Elimu Sekondari kuwa ni kuongeza shule. Alisema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2019 hadi 2021 shule 10 mpya zimeanzishwa zikiwamo, Ihanga Mbarali, Nyamakuyu, Mwakangaga, Ipwani, Kapunga, Itamboleo na Muwale.

"Tunajivunia mafanikio haya kwa sababu Rais Samia Suluhu Hassan ametupatia Sh. bilioni 1.8 kukamilisha ujenzi wa vyumba 94 vya madarasa sambamba na kutumwagia tena Sh. milioni 26 kujenga matundu 24 ya vyoo," alisema Shitindi

Naye Ofisa Elimu Mkoa wa Mbeya, Henry Hinju, aliwapongeza viongozi Mbarali kwa kuanzisha wiki ya elimu na kwamba imekuwa na tija kwani imeonyesha mabadiliko kutoka kufanya vibaya kwenye matokeo ya mitihani mbalimbali ya kitaifa.

Aliwashauri walimu kufanya kazi kwa moyo na kujitoa kuwafundisha watoto yale yanayopaswa ili kuwasaidia kufanya vizuri kwenye mitihani yao.



Mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya sekondari Mbarali, Geofrey Mlela (kulia), akionyesha ubunifu wa mfumo wa mawasiliano kati ya simu na redio kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Reuben Mfune (kushoto), wakati wa kilele cha wiki ya elimu, wilayani humo juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC akata mzizi mgogoro wa ardhi

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

EKARI 1,800 zilizoko katika Kata ya Nyanyala, mkoani Songwe zinatarajiwa kupimwa na kutumika kwa ajili ya shughuli za uzalishaji mali baada ya Mkuu wa Mkoa huo, Omary Mgumba, kufanya mkutano wa hadhara na wananchi, wafanyakazi wa kiwanda cha saruji na wadau wanaofanya shughuli za uchimbaji chokaa katika kijiji hicho.

Eneo hilo lenye hati namba 31 ambalo kwa muda mrefu limekuwa na mgogoro kati ya Kiwanda cha Saruji Mbeya juu ya nani mmiliki halali baina ya pande hizo ambao ulifikiwa mwafaka baada ya Mgumba kutoa taarifa ya kamati iliyoundwa kushughulikia suala hilo.

Mgumba alisema baada ya uamuzi wa kugawa ekari 1800, timu ya wataalamu iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan itapita kubaini maeneo yanayofaa kwa ajili ya kiwanda, kilimo, madini ya chokaa na eneo la wananchi ili kila mmoja abaki na eneo lake kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

"Serikali ilitoa hati namba 31 kwa kiwanda cha saruji wakati wako wananchi wanaomiliki kisheria wakiwa na hati za kimila kutokana na wengine kuachiwa ardhi hizo na babu zao sambamba na wachimbaji wa madini ya chokaa kupewa leseni halali ya kuendelea na shughuli za uchimbaji," alisema Mgumba.

Aliongeza kuwa kiwanda cha saruji Mbeya tayari kimeondoa kesi mahakamani baada ya kuona hakuna maslahi ya kuendelea nayo, wakati uwezo wa kumaliza mgogoro huo upo kwa kukaa meza moja na wananchi pamoja na wachimbaji wa chokaa.

Diwani wa Nanyala, George Musyani, alimshukuru Mgumba kwa kuitisha mkutano wa hadhara na kuja na mpango wa kupima eneo la ekari 1800 ambazo kiwanda cha saruji kinadai ni zake huku wananchi wakilitegemea kwa uzalishaji mali.

Mmoja wa wananchi waliohudhuria mkutano huo, Aneth Gambi, alisema ardhi ya Nanyala ni mali yao kwa kuwa walirithishwa na babu zao na kuzaliwa katika himaya hizo.

Julius Mwashilindi alisema kitendo cha kiwanda cha saruji Mbeya kuamua kumiliki ardhi hiyo bila kuwahusisha wananchi kupitia mkutano wa hadhara, ni chanzo cha mgogoro huo.

Vijiji vinne ambavyo ni Majimoto, Iwanga, Udinde na Malema vinaunda Kata ya Nanyala na kwamba vijiji vyote hivyo vimeunganishwa na huduma za kijamii.

## Wanafunzi kilimo waomba kupimiwa afya ya udongo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANAFUNZI wa Chuo cha Kilimo cha Mbalizi, wameomba wataalam kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, kupima afya ya udongo chuoni hapo ili kuendelea kuzalisha miche ya mazao kwa ubora unaotakiwa na kujiingizia kipato.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Getrude Mbembati alisema hitaji lao kwa sasa ni kupimiwa afya ya udongo chuoni hapo kwa ajili ya kuzalisha miche ya aina mbalimbali ikiwamo ya matunda kisha kuiuza kwa jamii inayowazunguka.

Mbembati alisema hadi sasa TARI -Uyole imewapatia miche na mbegu za aina mbalimbali huku wakiwapatia elimu ya namna ya kuotesha na kuhudumia mimea hiyo.

"Tunawashukuru TARI Uyole kwa kutupatia elimu ya kilimo bora pamoja na miche ambayo tunaendelea kuitunza hapa chuoni kwetu. Jambo la muhimu kwa sasa ni kuomba wataalam kupima udongo wa hapa ili kufahamu ni aina gani ya mbegu au miche inayostahili kupandwa hapa lakini pia tukibaini tatizo mtatusaidia kutengeneza afya ya udongo," alisema Mbembati.

Mkurugenzi wa TARI, Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema walibaini tatizo kubwa kwenye afya ya udongo, hivyo wameanzisha mradi wa kupima udongo katika mikoa minne ikiwamo Mbeya, Rukwa na Morogoro.

Alisema wataalam wa kituo hicho watakuwa wanapima udongo ili kujua tatizo lililopo pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao.

Mkuu wa Chuo cha Mbalizi Polytechnic College, Essau Mwasegile, alisema wamewajengea wanafunzi uwezo wa kuzalisha mbegu za aina mbalimbali na namna ya kuhudumia.

Alisema wamewajengea uwezo wa kwenda kuwafundisha wakulima namna bora ya kilimo bora pamoja na kuwapatia ushauri pindi wanapokabiliwa na matatizo katika uzalishaji.

Mmoja wa wahitimu wa chuo hicho, Gideon Malifimbo, alisema kwa sasa ana uwezo wa kutoa ushauri wa kilimo chenye tija kwa jamii yake na kwamba atakuwa mkulima wa mfano kwa kuwa atazalisha kwa kuzingatia utaalam.



HABARI ZANZIBAR

# Kipindi cha uchaguzi nchi nyingi huingia majaribu uvunjifu amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, amesema katika kipindi cha uchaguzi mkuu nchi nyingi duniani huingia katika majaribu yenye kuashiria uvunjifu wa amani na baadhi ya nchi hushindwa kudhibiti majaribu hayo na kupata athari za kiuchumi.

Aliyasema hayo jana katika hotuba yake iliyosomwa na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar, Shabani Abdallah Ramadhan, wakati akizindua mradi wa 'Amani yetu ni mshikamano wetu', wenye lengo la utatuzi wa migogoro na ujenzi wa amani Zanzibar ambao unasimamiwa na Jumuia ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), uzinduzi ambao umefanyika Mjini Zanzibar.

Alisema mradi huo utawajengea uwezo wanawake na vijana kupitia vyama vya siasa, viongozi wa dini na asasi za kiraia kwa njia ya midahalo ya wazi.

"Hii imekuja baada ya kuona kuwa mara nyingi panapotokea uvunjifu wa amani watu wa makundi haya ndiyo wanaoathirika zaidi na mimi niungane na lengo la mradi kwa kuwataka wasimamizi kuhakikisha wanayafuata malengo ya mradi huu kama yalivyokusudiwa," alisema.

Alisema midahalo hiyo iwanufaishe Wazanzibari kwa kuwaweka pamoja na isiwe chanzo cha migogoro bali ni sehemu ya kuelimishana na kujengeana uwezo na kuwa na uelewa wa pamoja wa dhana ya utatuzi wa migogoro.

Aliwataka viongozi wa vyama vya siasa, dini, asasi za kiraia, wadau wa maendeleo na waandishi wa habari kila mmoja kwa nafasi yake kuwa mstari wa mbele kuhubiri amani, kuendelea kupendana, kushirikiana, kuvumiliana na kuepuka vishawishi vya uvurugaji wa amani.

"Viongozi wa dini watumie majukwaa yao vizuri kwa waumini wao, wanasiasa nao wawatake wanachama wao kutojiingiza kwenye vurugu za kisiasa, waandishi wa habari kutumia vyombo vya habari vizuri kwani sote ni mashuhuda chombo cha habari ni kama kisu ukikitumia vizuri kitaleta faida na ukikitumia vibaya kitaleta madhara."

Aidha, alisema suala la utunzaji wa amani Zanzibar lina utamaduni wake na njia zake na kuwashauri wasimamizi wa mradi huo kuhakikisha wote watakaowatumia kusimamia midahalo wawe ni watu wanaojua Zanzibar, wenye uchungu na mapenzi ya nchi na wasitafute watu ambao badala ya kujenga amani wakawa wachochezi wa fujo na vurugu.

Mwakilishi wa Balozi wa Ujerumani Tanzania, Johannes Sperrtechter, alisema Ujerumani inasaidia maendeleo ya Zanzibar na inatambua changamoto za kiuchaguzi na mradi huo amani na maendeleo ya nchi.

Naye Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya kutoka Nairobi, Rashmi Thapa, wanaofadhili mradi huo, alisema kuwa imani yake mradi huo wa amani yetu ni mshikamano wetu utaleta mabadiliko katika utekelezaji wake.

Kwa upande wao washiriki katika uzinduzi wa mradi huo, wakiwemo viongozi wa dini, asasi za kiraia na viongozi wa vyama vya siasa kutoka CCM, CUF, ACT-Wazalendo na CHADEMA, walisema kuwa mradi huo ni muhimu kwa sababu Zanzibar imekuwa ikipambana na changamoto mbalimbali za masuala ya amani na migogoro inaishi katika jamii na kwamba ni muhimu kuwa na miradi kama hiyo ya kujenga maelewano ili kuwa na amani ya kweli.

"Nawashukuru sana wafadhili wetu wametuwezesha kushughulikia masuala nyeti yanayohusu jamii yetu na kwa sasa tulinde amani yetu na uchaguzi wa mwaka 2020 Zanzibar tumeishi katika amani na serikali ya umoja wa kitaifa imeleta amani katika siasa," alisema Askofu Agostino Shao wa Kanisa la Katoliki Zanzibar.

Mamhoud Mussa Wadi, Naibu wa Mufti Zanzibar, aliwapongeza waandaji wa mradi huo na kusisitiza amani ambayo ni sehemu ya usuluhishi wa migogoro hasa kabla, wakati na baada ya uchaguzi ambayo ni faida kubwa katika jamii.



Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi Zanzibar, Dk. Khalid Salum (wa pili kushoto), akizungumza na viongozi wa Serikali ya Mkoa wa Kusini, wakati akikagua maendeleo ya zoezi la uwekaji wa anuani za makazi katika shehia ya Jumbi, mkoani humo, jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi aipongeza Stanbic utekelezaji maendeleo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki ya Stanbic Tanzania kwa kuiunga mkono Zanzibar katika utekelezaji wa mikakati na mipango ya maendeleo iliyopangwa.

Dk. Mwinyi alitoa pongezi hizo Ikulu Zanzibar wakati alipofanya mazungumzo na uongozi wa benki hiyo, ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu, Kevin Wingfield.

Alisema azma ya Benki ya Stanbic ya kushirikiana na Serikali ya Zanzibar itasaidia kwa vile benki hiyo ina mpango wa kuanzisha tawi lake visiwani humo.

Aidha, Dk. Mwinyi aliuambia uongozi wa benki hiyo mikakati ya maendeleo iliyowekwa na serikali yake katika sera yake ya uchumi wa buluu, sekta za kijamii na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Alitaja fursa zilizopo katika uchumi wa buluu na kusisitiza kwamba serikali iko tayari kushirikiana na benki hiyo katika sera yake ya uchumi wa buluu hasa katika vipaumbele vyake ilivyoviweka.

Alivitaja miongoni mwa vipaumbele hivyo vilivyomo katika uchumi wa buluu kuwa ni sekta ya utalii, uvuvi wa bahari kuu, mafuta na gesi asilia, bandari, usafiri na usafirishaji.

Kwa upande wa sekta ya uvuvi, Dk. Mwinyi alieleza namna serikali ilivyokusudia kuwakomboa wavuvi kwa kuwapa utaalamu pamoja na nyenzo za kisasa hasa wavuvi wadogo ambao kwa muda mrefu kipato chao kilikuwa ni kidogo ikilinganishwa na shughuli wanazozifanya.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Wingfield alisema azma yao ni kufungua tawi lake Zanzibar hatua ambayo itasaidia kuunga mkono juhudi za serikali katika kujiletea maendeleo.

Alisema mikakati pamoja na shughuli za benki hiyo hasa katika kuunga mkono harakati za maendeleo katika sekta ya umma na binafsi ndani na nje ya Tanzania hasa ikizingatiwa kwamba benki hiyo ina matawi yake katika nchi mbalimbali duniani.

Wakati huo huo, Rais Mwinyi alifanya mazungumzo na wawekezaji kutoka Italia ambao wameonesha nia ya kuja kuwekeza Zanzibar kutokana na mazingira mazuri yaliyopo ikiwa ni pamoja na kuunga mkono sera ya uchumi wa buluu.

## Kamati Baraza la Wawakilishi yataka kilimo cha viungo kikaguliwe kuleta tija

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMATI ya Baraza la Wawakilishi ya kuchunguza hesabu za serikali imezitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo pamoja na Wizara ya Kilimo na Umwagiliaji kuhakikisha miradi ya kilimo cha viungo inakaguliwa ili kuleta tija kwa vijana kujikomboa na kujiajiri katika sekta hiyo.

Mwenyekiti wa Baraza la Wawakilishi wa kamati hiyo, Juma Ali Khatib, alisema hayo wakati kamati ilipofanya ziara kukagua miradi ya kilimo cha viungo inayotekelezwa na vijana na kuzungumza na uongozi wa Wizara ya Biashara.

Khatib alisema mradi wa viungo ni sehemu ya mikakati ya Serikali ya Zanzibar kuwawezesha vijana kujiajiri na kuingia katika kilimo cha mageuzi cha kibiashara.

Alisema kwa bahati mbaya miradi ya kilimo cha viungo cha biashara haijafanikiwa na kuyafikia malengo yake huku ikitumia fedha nyingi zilizotengwa na serikali akitoa mfano mradi wa pilipili kichaa huko Pangatupu, Mkoa wa Kaskazini B Unguja.

"Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya kuchunguza hesabu za serikali haijaridhishwa na utekelezaji wa mradi huo wa viungo ambao umelenga kuwakomboa vijana na kujiajiri kibiashara," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Dk. Islam Seif, aliwataka vijana kujikita katika kilimo cha viungo kutokana na kuwapo kwa soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Alisema kilimo cha viungo cha vanila na pilipili manga soko lake ni la uhakika na kinaweza kumkomboa mkulima kibiashara.

"Tayari zipo asasi za kiraia zimeanza kuwahamasisha wakulima kujikita zaidi katika kilimo cha mazao ya viungo cha kibiashara kupitia ufadhili wa jumuiya ya Ulaya (EU)," alisema Dk. Islam.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Maliasili, Mariyam Juma Sadalla, alisema kilimo cha viungo kimeanza kuleta matumaini mazuri kutokana na masomo ya shamba darasa yanayotolewa na wizara kwa vikundi vya wajasiriamali.

Alisema wakulima wa mazao ya viungo Unguja na Pemba tayari wamehamasika na kujikita katika kilimo hicho kwa mazao ya vanila na bei yake ni nzuri katika soko la dunia.

## HABARI KIMATAIFA

UCHAGUZI MKUU KENYA 2022:



Viongozi wa vyama 12 vya siasa vilivyoungana jana nchini Kenya ikiwa ni hatua ya kuelekea uchaguzi mkuu. **PICHA: NATION MEDIA GROUP**

# Mamlaka ya anga yawaonya marubani

**Nairobi,** KENYA

KUELEKEA uchaguzi mkuu Agosti, mwaka huu, Kenya imewataka marubani na waendeshaji helikopta, kuchukua tahadhari wakati wa kutua au kuruka hasa kwenye mikusanyiko ya kisiasa.

Wameambiwa wataadhibiwa iwapo itatokea kwenye shughuli hatari ndege zinapotua au kuruka wakati wa mikusanyiko ya kisiasa.

Katika barua yenye onyo kali kwenda kwa wasimamizi na wahudumu wa helikopta, kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Kenya (KCAA), imeibua wasiwasi kwamba utendaji kazi wa usafiri wa helikopta, unahatarisha maisha ya watu.

Onyo hilo linajiri siku chache baada ya 'chopa' iliyokuwa imembeba kiongozi wa ODM Raila Odinga na viongozi wengine kupigwa mawe na vijana katika ghasia wakati wa mazishi ya Mzee Jackson Kibor, katika shamba la Samitui, Kaunti ya Uasin Gishu, Aprili Mosi, mwaka huu.


KCAA ilionya kwamba marubani na wafanyakazi wa helikopta na wote wanaohusika katika matukio kama hayo kuanzia sasa, watawajibika binafsi.

KCAA iliwaandikia mameneja na marubani helikopta Aprili 6, mwaka huu, kufuatia visa kadhaa vilivyohusisha watu kuning'inia kwenye helikopta zilipokuwa zikipaa na mengine ambayo helikopta zilipaa huku umati wa watu wakiwa wamesimama karibu, ikisema ni hatari.

"Ni jukumu la mwendeshaji wa helikopta kuhakikisha kuwa ndege hiyo inaendeshwa kwa usalama na usalama ikiwa ni pamoja na usalama wake ardhini.

"Kwa hivyo, ili kufikia lengo hili, marubani wa helikopta wanatakiwa kufanya mipango ya kuhakikisha usalama wa ndege inapotua.

> "Kuwajibika ni katika shughuli zozote za hatari kwa marubani na wafanyakazi, ambao hufanya maamuzi kuhusu mahali pa kutua na pia maamuzi ya wakati wa kuruka.



Raila Odinga



William Ruto

"Katika maeneo yasiyo na rubani mipango hiyo inaweza kufanywa kupitia utawala wa ndani na Huduma ya Kitaifa ya Polisi," barua hiyo ya Mkurugenzi Mkuu wa KCAA, Gilbert Kibe, ilisema.

"Kuwajibika ni katika shughuli zozote za hatari kwa marubani na wafanyakazi, ambao hufanya maamuzi kuhusu mahali pa kutua na pia maamuzi ya wakati wa kuruka."

Kibe alisema: Mwongozo ni kutua na kuruka angalau kilomita tatu kutoka maeneo ya shughuli na kuhakikisha angalau eneo la mita 30, lisiwe na watu wowote.

"Kupandisha mtu katikati ya umati wa watu au mahali ambapo hakuna umbali wa kutosha kati ya ndege na umati ni ukiukaji mkubwa wa sheria za uendeshaji salama wa ndege."

Mamlaka pia iliwataka marubani hao kuwajulisha wateja wao wengi wao ikiwamo wanasiasa, kutojihusisha na shughuli zinazohatarisha utendaji kazi wa ndege, ikiwa ni pamoja na kuhutubia umati wa watu karibu na ndege au kujihusisha na shughuli za kuvuta umati wa watu wakiwa ndani au karibu na ndege.

Mamlaka iliongeza kwamba, itachukua hatua kwa wahusika wa usafiri huo wakibainika kufanya uzembe, hivyo kuhatarisha maisha.

"Marubani wanakumbushwa kuwa ni wajibu wao binafsi chini ya idhini ya operesheni iliyotolewa na leseni walizonazo ili kuhakikisha usalama wa ndege na abiria wake pamoja na watu walio chini kabla na wakati wa kupaa," KCAA ilisema.

Ilisema kuna taratibu za uendeshaji zilizoandikwa (SOPs) na maagizo ya kazi na wafanyakazi wanaohusika katika kusafirisha VIP wakati wa kampeni kabla ya uchaguzi wa Agosti 9, mwaka huu.

Mwanzoni mwa mwezi huu, Raila Odinga anayewania urais kupitia Azimio la Umoja-One Kenya alilaumu shambulio dhidi yake akiwa katika helkopta eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu.

Raila ameendelea na kampeni kuelekea uchaguzi mkuu Agosti mwaka huu.

Alisema kundi la vijana lilimvamia wakati akiondoka eneo hilo kuelekea Ortum, Alale na Lomut, kuendelea na kampeni.

Alidai kwamba mawe yalirushwa akiwa pamoja na ujumbe wake, hata wakati akielekea kupanda helikopta mawe yaliendelea kurushwa.

"Sisi hatujapiga mtu yeyote. Wala hatujafanya fujo pahali popote, tunalaani. Jana mimi nimeona vioja. Vijana wanakuja sisi tulitoka kutoa pole kwa familia alafu wakaanza kupiga magari yetu mawe.

"Mawe yalinyesha kama mvua kwa gari langu. Wakipiga, nikauliza ni nini inafanyika. Vijana wakangoja nikiingia kwa ndege alafu nikaona mtu anarusha mwamba mkubwa na sikuwa na pahali pa kuenda. Nilishangaa, ni mambo gani haya. Jamaa walitaka kuua sisi."

Baada ya tukio hilo Rais Uhuru Kenyatta alilaani kitendo hicho, akisema ni hatari kwa usalama wa nchi, huku watuhumiwa 17 wakifikishwa mahakamani Eldoret wakihusishwa na shambulizi dhidi ya mgombea urais kupitia muungano wa Azimio la Umoja-One Kenya, Raila Odinga, lililotokea eneo la Kabenes, Kaunti ya Uasin Gishu, mwishoni mwa wiki.

Washukiwa hao wanadaiwa kuhusika na shambulizi la kupiga mawe helikopta iliyokuwa imembeba Raila, ambaye ni kiongozi wa chama cha ODM, eneo la shamba la marehemu Mzee Jackson Kibor la Samitui, muda mfupi baada ya mazishi.

Miongoni mwa mashtaka dhidi yao ni pamoja na jaribio la mauaji, uchochezi wa ghasia, uharibifu wa mali na uvunjifu wa amani.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# MOROCCO ATANGAZWA TENA KOCHA MKUU Z'BAR HEROES

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), limemrejesha kwa mara nyingine Hemed Morocco kuwa kocha mkuu wa timu ya Taifa ya Zanzibar 'Zanzibar Heroes'.

Morocco atakinoa Kikosi cha Zanzibar Heroes katika michuano mbalimbali ambayo Zanzibar itapata nafasi ya kushiriki timu ikiwamo ile ya CECAFA.

Pia, ZFF imetangaza majina ya makocha wengine akiwamo Ali Mohammed Ameir ambaye anakuwa kocha mkuu wa timu za Taifa za Vijana Zanzibar.

Ameir aliwahi kuwa kocha wa timu mbalimbali hapa visiwani Zanzibar ikiwamo timu ya Mwembe Makumbi City inayocheza Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja.


MwIngine aliyetangazwa ni Abdulmutik Ali Haji kuwa kocha mkuu wa timu za Taifa za Wanawake Zanzibar, ' Zanzibar Queens'.

**Katibu Mkuu wa ZFF, Hussein Ahmada Vuai, alisema makocha hao wamepatikana baada ya kupitia taratibu zote zilizohitajika.**

Alisema wadau wa soka Zanzibar waendelee kutoa mchango wao wa dhati na kuendelea kipeana moyo ili soka visiwani hapa linyanyuke, lakini pia kuzipata timu za taifa zitakazotoa ushindani mkubwa katika mashindano mbalimbali watakayoshiriki.

Zanzibar si mwanachama wa Fifa wala CAF, hivyo mashindano ambayo inashiriki kwa kupeleka timu ya taifa ni yale ya CECAFA, mashindano ya nchi wasio wanachama wa Fifa (CONIFA) pamoja na mashindano ya nchi za visiwa.

## 'UMETIKI'...




Mkazi wa Kibiti mkoani Pwani, Yasin Kingwande (katikati), akionyesha mtindo wa ushangiliaji wa mshambuliaji nyota wa Yanga, Fiston Mayele, baada ya kutupia bao muhimu kwenye Ligi Kuu dhidi ya Azam FC Jumatano iliyopita, na kuufanya mkeka wake kufanikiwa. Wengine pichani ni marafiki zake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Coastal wajiandaa nusu fainali FA Cup

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mikwaju ya penalti 5-4 dhidi ya Kagera Sugar juzi, kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga, Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda amesema wanajiandaa kucheza mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA bila ya kuangalia ni nani watakayecheza naye.

Kocha huyo ambaye timu yake ilimaliza dakika 90 matokeo yakiwa sare ya bao 1-1 dhidi ya wapinzani wao, ameseme yeyote yule atakayeingia kwenye hatua hiyo wao wako tayari kucheza naye, iwe timu kubwa au ndogo.

"Huyo atakayejaaliwa kuingia nusu fainali ndiyo tutakwenda kucheza naye, hatuchagui wa kucheza naye kwa sababu sisi hatujapanga na wala hatupangi ratiba, kazi yetu ni kucheza tu. Kimsingi ni kwamba sasa tunajiandaa kwenda kucheza nusu fainali na si kuangalia tutakayecheza naye," alisema straika huyo wa zamani wa timu hiyo.

Akizungumzia mechi hiyo, alisema timu yake ilicheza kimkakati zaidi kwa sababu michezo ya mtoano ni tofauti na ligi.

"Hizi mechi huwa ni ngumu na zinachezwa kwa maelekezo, hazihitaji pointi, kwa hiyo tunacheza kimkakati zaidi. Unajua siku zote ukitanguliwa kufungwa na wewe ulikuwa na matumaini ya kuanza kufunga bao, kwa vijana wadogo kama wale, ni lazima kocha usionekane kushtuka, la sivyo utawachanganya, na ndivyo nilivyofanya, mapumziko niliwaambia jamaa wanaongoza, hawajashinda na kweli tunarudisha bao na kushinda kwa mikwaju ya penalti," alisema.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Francis Baraza, alikiri kuwa mabeki wake walifanya uzembe mpaka Coastal Union wakarudisha bao ambalo walifunga awali.

# Yanga Sc: Hatuachi kitu msimu huu

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufuzu nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam Sports (ASFC), maarufu FA Cup kwa kuitoa Geita Gold FC kwa mikwaju ya penalti 7-6 kufuatia sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90, uongozi wa Yanga umesema wako tayari kukutana na timu yoyote katika hatua hiyo kwa kuwa wanahitaji makombe yote wanayoshiriki msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa Yanga, Senzo Mazingisa, alisema wanatakiwa kufanya vizuri katika mashindano wanayoshiriki msimu huu, Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho.

Alisema wanahitaji kupambana kuhakikisha wanafanya vizuri, kwa kuwa hayo ndiyo malengo yao kutokana na kudhamiria kuchukua makombe yote.

"Wachezaji wanatakiwa kupambana na wanatakiwa kufahamu ili kuwa mabingwa, basi tunatakiwa kushinda michezo mikubwa, baada ya kuwafunga Azam FC na Geita Gold na (baadaye tukiifunga) Simba, tutakuwa tunaenda kufikia malengo yetu," alisema Senzo.

Alisema Yanga imekuwa na mabadiliko makubwa na msimu huu watahakikisha wanafanya vizuri na kutoacha kitu katika mpango wao wa kuchukua makombe yote.

"Msimu huu tumejiandaa vizuri na tutahakikisha hatuachi chochote kwa sababu, hatuna presha na yeyote tutakayekutana naye iwe Simba au Pamba, tuko tayari kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kutoacha chochote katika michuano iliyopo mbele yetu," alisema Senzo.

Naye Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema kwa sasa wanaendelea na maandalizi ya kuhakikisha wanafanyia kazi madhaifu yao kwa ajili ya michezo yao ijayo.

Alisema hawana presha na michezo yao ijayo ikiwamo wa nusu fainali ya Kombe la Shirikisho kwa kukiandaa kikosi kukabiliana na timu yoyote ambayo watakutana nao katika hatua inayofuata.

"Tumefurahi kuingia katika hatua ya nusu fainali, tunaenda kujiandaa na michezo ijayo bila kujali tunakutana kati ya Simba au Pamba, kikubwa tunajiandaa kuhakikisha msimu huu tunafikia malengo yetu ya kutwaa ubingwa na Kombe la Shirikisho," alisema Kaze.

Yanga inaongoza ambayo sasa inasubiri kukutana na mshindi kati ya Simba na Pamba kwenye nusu fainali ya Kombe la Shirikisho, pia inaongoza msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 51 baada ya kucheza mechi 19, bado mechi 11 kumaliza msimu huu wa Ligi Kuu huku watani wao wa jadi, Wekundu wa Msimbazi hao wakiwa nafasi ya pili na alama zao 41.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### POGBA ATAKIWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain imemfanya kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, kama kipaumbele chao kumsajili. (***Footmercato***)

### NEVES AWINDWA ARSENAL
KIUNGO wa Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, anawaniwa na Arsenal. (***Sky Sports***)

### LEWANDOWSKI SAFI BARCA
STRAIKA wa Poland, Robert Lewandowski anapanga kuondoka Bayern Munich kipindi cha majira ya joto na ameshafikia makubaliano binafsi na Barcelona. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, mkataba wake na Bayern unamalizika kipindi cha majira ya joto 2023. (***TVP Sport, via Mail***)

### MERINO HUYOOO UNITED
KLABU ya Manchester City inawania kumsajili nyota wa Real Sociedad, Mikel Merino mwenye umri wa miaka 25, ambaye ada yake ni pauni milioni 50. (***El Confidencial, via Manchester Evening News***)

### FERNANDEZ ATEGEWA CITY
PEP Guardiola pia ametega ndoana zake kwa kiungo wa River Plate, Enzo Fernandez mwenye umri wa miaka 21. (***Goal***)

### KULUSEVSKI KUBAKI SPURS
KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, anataka kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa Sweden, Dejan Kulusevski, mwenye umri wa miaka 21 ambaye anacheza kwa mkopo kutoka Juventus. (***Calciomercato***)

### LEICESTER KWA YILMAZ
MLINZI wa kushoto wa Besiktas, Ridvan Yilmaz mwenye umri wa miaka 20, anawaniwa na Leicester City. (***TGRT Haber***)

### NUNEZ KUONDOKA BENFICA
STRAIKA wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, ataondoka Benfica kipindi cha majira ya joto. (***Fabrizio Romano***)

### ORIGI KUTUA MILAN
STRAIKA wa Liverpool na Ubelgiji, Divock Origi mwenye umri wa miaka 26, amekubali kujiunga na AC Milan kipindi cha majira ya joto. (***Sport Mediaset, via Football Italia***)

### INGS, BISSOUMA KUPISHANA
STRAIKA wa Aston Villa, Danny Ings mwenye umri wa miaka 29, anaweza kupelekwa Brighton katika dili litakaomhusisha kiungo wa Mali mwenye umri wa miaka 25, Yves Bissouma. (***Mirror***)

### TROSSARD ATAKIWA NEWCASTLE
WINGA wa Brighton na Ubelgiji, Leandro Trossard mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na Newcastle United. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BENZEMA STRAIKA BORA ZAIDI DUNIANI - PIRES

●●● Yeye na Robert Lewandowski wote wanashiriki nafasi moja kama washambuliaji bora kwa...

**PARIS,** UFARANSA

HAKUNA mshambuliaji bora duniani kwa sasa kuliko straika wa Real Madrid, Karim Benzema, kwa mujibu wa Robert Pires.

Pires anaamini kuna mengi zaidi kutoka kwa mshambulizi huyo mwenye umri wa miaka 34, anapoiongoza Real Madrid kutwaa taji la 35 la LaLiga.

Pires, akizungumza kama balozi wa LaLiga Global Partners LiveScore, alisema: "Karim Benzema ni mchezaji wa ajabu. Ni kama mvinyo ayekomaa na umri, anazidi kuwa bora na bora.

"Siku zote huwa nawaambia mashabiki, tunapokuwa na wachezaji kama Karim tunahitaji tu kufurahia kuwatazama wakicheza.

"Mchezaji mzuri, mshambuliaji mzuri ambaye anaweza kufunga mabao mengi, wanaweza kuleta mabadiliko.

**"Lakini si msimu huu pekee. Imekuwa kwa muda mrefu sana.**

"Baadhi ya watu husema: 'Wow, Karim Benzema, yeye ni mchezaji mzuri sasa'. Ninasema: 'njoo, amka, si tu imekuwa hivyo kwa msimu mmoja, amecheza hivi kwa misimu tisa au 10 akiwa na Real Madrid.'

"Watu hawawezi kufikiria shinikizo linaloletwa. Ndiyo maana nasema yeye ni kama divai nzuri, anayekomaa na uzee, anaendelea kuwa bora na bora.

"Ningesema yeye na Robert Lewandowski wote wanashiriki nafasi moja kama washambuliaji bora zaidi duniani hivi sasa." Hivi majuzi Benzema alimpita gwiji wa 'Los Blancos', Alfredo Di Stefano aliyefunga mabao 308 katika maisha ya soka kwa klabu hiyo na anabakiza saba tu ya mabao 323 ya Raul.

Mchezaji - mwenza wa zamani na Benzema, Cristiano Ronaldo anaongoza kwenye chati ya wafungaji mabao 450 na Pires anaamini kwamba muda wa Mreno huyo wa Madrid ulisaidia kumtengeneza Benzema kama mchezaji.

Pires alisema: "Nadhani alijifunza mengi kutoka kwa Cristiano Ronaldo huko Real Madrid. Na sasa yeye si tu mshambuliaji mzuri, ni kiongozi mwenye nguvu na sifa zote za uongozi.

"Karim alipomwona Cristiano Ronaldo akiondoka Real Madrid, alichukua majukumu mengi.

"Yeye ni nahodha bila shaka (Marcelo hayupo) na unapokuwa nahodha wa Real Madrid una jukumu kubwa. Lakini hakuwa na hofu kuchukua jukumu hilo na tangu Cristiano Ronaldo aondoke, Karim amekuwa bora zaidi."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,144

MECHI KALI
ATLETICO MADRID
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 4.32
X | 3.45
2 | 1.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LIVERPOOL HAIFIKIRII MATAJI 4 – ROBERTSON



**LIVERPOOL,** England

WACHEZAJI wa Liverpool hawajadili uwezekano wa kupata mataji manne kwa sababu mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England ziko nje ya mikono yao, amesema Andy Robertson.

Manchester City imeipita pointi moja Liverpool kwenye msimamo baada ya timu hizo kutoka sare ya mabao 2-2 katika mchezo wa kusisimua uliopigwa kwenye Uwanja wa Etihad, Jumapili.

'Wekundu' hao watacheza tena na Man City Jumamosi kwenye nusu fainali ya Kombe la FA, ambapo vijana wa Jurgen Klopp walishanyanyua Kombe la Carabao mapema msimu huu.

Liverpool pia wanaweza kukutana na kikosi cha Pep Guardiola katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa wataishinda Benfica na Atletico Madrid katika robo-fainali yao, kwenye mechi zao za pili, leo Jumatano.

Mohamed Salah alisema kabla ya mechi ya City kwamba Liverpool ilitaka kushinda mataji yote manne, lakini Robertson anasisitiza kwamba hakuna mazungumzo kama hayo kati ya wachezaji.

"Kwa kweli tunazungumza tu kuhusu mchezo unaofuata. Unavyokuja. Huwezi kuangalia mbele sana, unafikiria mchezo unaofuata na hiyo ni Benfica kisha tusonge mbele kutoka hapo. Hakika hakuna gumzo kama hilo kwenye chumba chetu cha kubadilishia nguo," alisema Robertson.



# *Neville: Hakuna uhakika Hag atatua Man United*

**MANCHESTER,** England

GARY Neville amesema hakuna uhakika kwamba, Erik ten Hag atataka kuchukua nafasi ya kuwa kocha mkuu wa Manchester United.

Kocha huyo wa Ajax, Ten Hag ameripotiwa anatakiwa United kuchukua nafasi ya kocha wa muda, Ralf Rangnick mwishoni mwa msimu huu.

'Mashetani Wekundu' hao wanaweza kukosa nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, kwani wapo nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kufungwa bao 1-0 na Everton, Jumamosi.

United haijashinda taji lolote tangu mwaka 2017 na kwa sasa wanajipanga kukijenga upya kikosi chao.

Neville aliwalenga wachezaji baada ya kufungwa na ingawa mlinzi huyo wa zamani wa United ana matumaini watarudi kwenye kiwango chao, hatashangaa kama Ten Hag ataamua kuachana na mpango wa kutua hapo Old Trafford.

4,195,580

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/04/2022 | 17:00 | Watford vs Brentford | 2.66 | 3.16 | 2.66 |
| 02. 16/04/2022 | 17:15 | Alaves vs Rayo Vallecano | 2.57 | 3.03 | 2.93 |
| 03. 16/04/2022 | 17:30 | Manchester City vs Liverpool | 2.35 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 16/04/2022 | 18:00 | St Etienne vs Brest | 2.31 | 3.21 | 3.11 |
| 05. 16/04/2022 | 20:00 | Dijon vs AC Ajaccio | 2.31 | 3.10 | 3.15 |
| 06. 16/04/2022 | 20:00 | Nimes vs Sochaux | 2.44 | 3.15 | 2.90 |
| 07. 16/04/2022 | 20:00 | Valenciennes vs Le Havre | 2.65 | 3.15 | 2.65 |
| 08. 17/04/2022 | 16:00 | Metz vs Clermont Foot | 2.65 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 17/04/2022 | 16:15 | Newcastle vs Leicester | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 10. 17/04/2022 | 18:30 | Union Berlin vs Eintracht Frankfurt | 2.38 | 3.26 | 2.91 |
| 11. 17/04/2022 | 20:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.71 | 3.41 | 2.46 |
| 12. 17/04/2022 | 20:30 | Giresunspor vs Besiktas | 2.88 | 3.28 | 2.36 |
| 13. 17/04/2022 | 22:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 3.19 | 3.19 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 13/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4028 | Gamba Osaka vs Oita Trinita | 1.92 | 3.36 | 3.56 |
| 13:00 | 4520 | Sagan Tosu vs Kashiwa Reysol | 2.64 | 3.13 | 2.49 |
| 13:30 | 1269 | Nagoya Grampus vs Sanfrecce Hiroshima | 2.25 | 2.87 | 3.25 |
| 14:00 | 5259 | Fiorentina Youth vs US Lecce youth | 1.98 | 3.60 | 3.16 |
| 14:00 | 5533 | Sampdoria Youth vs Roma Youth | 3.10 | 3.64 | 1.99 |
| 15:00 | 1936 | Spartak Tuimazy vs Dinamo Barnaul | 2.97 | 3.36 | 2.15 |
| 15:00 | 4038 | AEK Athens B vs Rhodos FC | 1.77 | 2.76 | 5.82 |
| 15:00 | 5032 | Jimma Aba Jifar vs Fasil Kenema | 8.75 | 3.99 | 1.36 |
| 15:00 | 5636 | Halide Edip vs 76 Igdir Belediyespor | 11.66 | 5.25 | 1.21 |
| 15:30 | 1902 | Africain vs CS Chebba | 1.52 | 3.65 | 7.40 |
| 15:30 | 2005 | US Monastir vs Sportive Zarzis | 1.63 | 3.11 | 6.03 |
| 15:30 | 2151 | ES Sahel vs Olympique de Beja | 1.46 | 3.45 | 7.98 |
| 15:30 | 3981 | Torre Neapolis vs Virtus Francavilla | 2.35 | 3.05 | 3.15 |
| 15:30 | 5627 | AS Slimane vs Avenir Rjich | 1.40 | 3.75 | 8.37 |
| 16:00 | 1476 | Juventus Youth vs Pescara Youth | 1.21 | 5.83 | 9.52 |
| 16:00 | 2919 | Wakiso Giants FC vs Express FC | 2.81 | 3.01 | 2.43 |
| 16:00 | 4587 | Tooro United vs Bright Stars | 4.87 | 3.36 | 1.68 |
| 16:00 | 4692 | Bologna Youth vs Sassuolo Youth | 2.96 | 3.74 | 2.02 |
| 16:00 | 5131 | Kafue Celtic FC vs Zanaco | 2.86 | 2.62 | 2.71 |
| 17:00 | 2232 | Projek Fam-Msn vs Kelantan United FC | 6.24 | 4.29 | 1.41 |
| 17:00 | 2431 | Sagrada Esperanca vs Wiliete SC | 1.61 | 3.75 | 5.60 |
| 17:00 | 2590 | CD Lunda Sul vs Primeiro De Agosto | 2.57 | 2.86 | 2.77 |
| 17:00 | 5007 | MSK Namestovo vs Partizan Bardejov | 5.62 | 4.36 | 1.44 |
| 17:30 | 3175 | Dukla Prague vs FK Viktoria Zizkov | 1.68 | 3.75 | 4.18 |
| 17:30 | 3218 | Graffin Vlasim vs Sparta Prague B | 2.31 | 3.26 | 2.77 |
| 17:30 | 3687 | Fotbal Trinec vs Varnsdorf | 2.49 | 3.37 | 2.49 |
| 17:30 | 4004 | Vyskov vs Pribram | 2.34 | 3.21 | 2.77 |
| 17:30 | 5420 | Paide Linnameeskond vs Tallinna JK Legion | 1.10 | 7.60 | 16.57 |
| 17:30 | 5969 | MFK Chrudim vs Taborsko | 2.01 | 3.16 | 3.50 |
| 17:45 | 5465 | HB Chelghoum Laid vs JS Kabylie | 3.40 | 2.77 | 2.25 |
| 18:00 | 1209 | NK Ilirija vs ND Beltinci | 2.47 | 3.20 | 2.85 |
| 18:00 | 2309 | Wolkite City FC vs Bahir Dar Kenema FC | 3.31 | 2.72 | 2.32 |
| 18:00 | 2715 | Ergotelis vs Kallithea FC | 3.30 | 2.77 | 2.29 |
| 18:00 | 5360 | Trans Narva vs Tallinna Kalev | 1.45 | 4.28 | 5.65 |
| 19:00 | 2971 | Opava vs SK Prostejov | 1.65 | 3.75 | 5.00 |
| 19:00 | 4820 | Bron Radom vs Legia II Warszawa | 3.89 | 3.55 | 1.78 |
| 19:00 | 5556 | Ludogorets Razgrad vs Levski Sofia | 1.61 | 3.84 | 4.56 |
| 19:00 | 5828 | Jihlava vs SK Lisen | 2.87 | 3.36 | 2.20 |
| 19:30 | 2533 | Levadia Tallinn vs Nomme Kalju | 1.70 | 3.85 | 3.99 |
| 19:30 | 3342 | Randers vs Midtjylland | 3.08 | 3.38 | 2.20 |
| 20:00 | 3749 | Zbrojovka Brno vs Usti Nad Labem | 1.23 | 5.25 | 10.70 |
| 21:15 | 1160 | Al Nasr Salalah vs Saham Club | 1.63 | 3.65 | 5.40 |
| 21:15 | 2907 | Rustaq Club vs Nizwa | 1.58 | 3.54 | 5.43 |
| 21:15 | 4388 | Oman Club vs Al Seeb | 6.20 | 3.30 | 1.66 |
| 21:20 | 3285 | AL Adalh vs Al Orubah | 2.19 | 2.95 | 3.65 |
| 21:30 | 4363 | Kazma SC vs AL Tadamon | 1.36 | 5.00 | 7.60 |
| 21:30 | 5614 | AL Kawkab vs AL Jeel | 2.27 | 2.90 | 3.50 |
| 21:40 | 3557 | Najran SC vs Al Wehda | 3.40 | 2.85 | 2.36 |
| 22:00 | 1175 | Atletico Madrid vs Manchester City | 4.32 | 3.45 | 1.82 |
| 22:00 | 1506 | Liverpool vs Benfica | 1.27 | 5.99 | 8.78 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MKAZI MOROGORO ASHINDA SH. MILIONI 15 ZA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Lukobe mkoani Morogoro, George Kimaro ameibuka mshindi wa kufunga Kampeni ya Bet Bonanza ya Sportpesa, baada ya kujishindia kitita kikubwa zaidi cha shilingi 15,888,000 katika droo ya mwisho ya Bet Bonanza ambayo ilifikia tamati jana.

Katika droo hiyo ambayo pia imehusisha washindi wa droo ya shilingi milioni moja moja kwa kila mtandao, mchezaji Twaha Mustafa alishinda milioni moja kupitia mtandao wa Vodacom akitokea Arusha, mshindi mwingine akiwa ni Mohamed Mustafa wa Selous akipatikana kupitia Airtel na mshindi wa mwisho Thomas Uzuri wa Rukwa Sumbawanga alipatikana kupitia mtandao wa Halotel.

Droo hiyo ni sehemu ya promosheni ya Bet Bonanza ya Sportpesa, na pia ni muendelezo wa zawadi ambazo zilikuwa zinatolewa katika kipindi hiki cha ligi mbalimbali zinazoendelea kwa ushirikiano na Kampuni za simu za Vodacom, Airtel na Halotel.

Akizungumza baada ya droo iliyochezeshwa Makao Makuu ya Sportpesa jijini Dar es Salaam jana, Meneja Uhusiano na Mawasiliano Sportpesa, Sabrina Msuya, alisema jana ilichezeshwa droo ya tano na ya mwisho katika Kampeni ya Bet Bonanza, ambapo wateja wa Halotel, Airtel na Vodacom wamejishindia vitita hivyo vya mamilioni ya shilingi ya shilingi kwa siku siku 35 mfululizo.

"Leo (jana), ndio imekuwa siku yetu ya mwisho ya kampeni yetu ya Bet Bonanza, muda mfupi uliopita imechezeshwa droo ambapo mteja wetu kupitia mtandao wa Vodacom George Kimaro (23), ambaye pia amemaliza chuo kikuu, amejishindia Sh. 15,888,000, ambayo ndio ilikuwa zawadi kubwa kabisa na wengine watatu kutoka Airtel, Halotel na Vodacom.

Akitoa neno la pongezi kwa washindi; Kimaro pamoja na Mustafa, Meneja Biashara Huduma ya Mpesa-Vodacom, Kelvin Nyanda, aliwataka washindi hao kutumia vizuri fedha hizo kwa kuwa kipindi hiki ni cha sikukuu.

Akiwakilisha kutoka Halotel, Afisa Masoko, Roxana Kadio amempongeza Thomas Adam na pia washiriki wote walioshiriki kwa kutumia mtandao wa Halotel, na hata kama kuna ambao hawakushinda akiwataka wasikate tamaa, kwani nafasi za ushindi zipo nyingi na wakijaaliwa watashirikiana na Sportpesa kwenye promosheni nyingine ambayo itajitokeza siku za usoni.

"Nawashukuru wale wote ambao tumekuwa pamoja kwa siku zote 35 za promosheni hii na pia nawapa hongera washindi wote walioshinda katika kipindi cha promosheni," alisema.

Naye mwakilishi kutoka Airtel, Aggrey Charles, alimpongeza Mustafa na kumhimiza kuendelea kucheza na SportPesa.

Akiwakilisha Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ambao ndio walikuwa wasimamizi wa promosheni hii, Elibariki Sengasenga, amewapongeza SportPesa kwa kuendesha promosheni hii kwa umahiri mkubwa pamoja na washindi wote kwa ujumla kwa kushiriki na pia kuwataka kucheza kwa kuzingatia vigezo vya ushiriki katika mchezo huu.

"Ninapenda kuwaasa Watanzania mcheze kwa kuzingatia vigezo na masharti ya promosheni mnazoshiriki na pia msisite kuwasiliana nasi kwa msaada zaidi muda wowote ambao mtakuwa na Jambo mnalohisi linahitaji msaada wetu," alisema.

Promosheni hii ilizinduliwa rasmi Machi 8, mwaka huu ikijumuisha zawadi za Sh. 20,000 kila siku, Sh. milioni moja moja kwa washindi watatu kila wiki na Sh. milioni 15.8 siku ya kufunga kampeni ambayo ni jana.



Baadhi ya wawakilishi wa Promosheni ya Bet Bonanza kutoka SportPesa ni Sabrina Msuya (katikati), Airtel Money, Aggrey Charles (wa pili kushoto), Mpesa, Frank Nyanda (wa pili kulia) pamoja na Halo Pesa, Roxana Kadio (wa kwanza kulia), wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kuchezeshwa droo ya kumtangaza mshindi wa shilingi 15,888,000 kwenye promosheni hiyo iliyomalizika rasmi jana. Wa kwanza kushoto ni Frank Charles Gibebe mtangazaji kutoka SportPesa. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mahadhi aomba radhi kukosa penalti

**Na Dennis Fussi**

MSHAMBULIAJI wa Geita FC, Juma Mahadhi, amewaomba msamaha wachezaji wenzake na viongozi wa timu hiyo kutokana na kitendo chake cha kukosa mkwaju wa penalti katika mchezo wa robo fainali wa Kombe la FA dhidi ya Yanga.

Geita walitolewa kwa mikwaju ya penalti kwenye mchezo huo uliopigwa Jumapili katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mahadhi ameliambia gazeti hili kuwa anajihisi kuchanganyikiwa, kila tukio lile linapomjia akilini, kitu ambacho kinamfanya ajute na kukosa furaha.

"Malengo yetu ilikuwa ni kuitoa Yanga na kutinga nusu fainali, tulifanya maandalizi mazuri na uongozi ulitupatia kila kitu," alisema.

"Najihisi kuwaangusha wenzangu na uongozi, naomba wanisamehe binafsi inaniuma sana."


Mshambuliaji huyo aliyewahi kucheza Yanga, amesema baada ya kushindwa kufikia malengo wanapaswa kurudisha nguvu kwenye ligi, ili kumaliza msimu katika nafasi za juu.

Amesema ukitoa ubingwa na nafasi ya pili, nafasi zilizobaki timu yoyote inaweza kumaliza, hivyo cha msingi ni kuhakikisha wanapata matokeo kwenye mechi zao zilizobaki za ligi hiyo.

Michezo

Jumatano Aprili 13, 2022

Nipashe




'Benzema straika bora zaidi duniani'

UKURASA 21

# Simba yataka kuvunja rekodi CAF

## ●●● Viongozi watangaza mazito kuelekea kuivaa Orlando kwa Mkapa...

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha wawakilishi pekee wa nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba, ikiendelea na maandalizi mazito kambini kuelekea mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini, viongozi wa klabu hiyo ya Tanzania, wametangaza mazito.

**Simba itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumapili wiki hii majira ya saa 1:00 usiku kuikaribisha Orlando Pirates katika mechi ya robo fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Kuelekea mchezo huo, viongozi wa Simba wamezindua kampeni kabambe ya kuhamasisha mashabiki wa timu hiyo kuhudhuria mechi hiyo ya Jumapili na kuujaza uwanja ili kuongeza morali kwa wachezaji kuweza kupata ushindi mnono, hiyo ikiwa ni baada ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kuruhusu mashabiki 60,000 kuingia uwanjani kushuhudia mchezo huo.

Akizungumza katika ufunguzi wa kampeni ya hamasa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mwina Kaduguda, alitoa ahadi nzito baada ya kueleza kuwa kama kunahitajika mtu afe ili Simba itwae Kombe la Shirikisho Afrika basi yupo tayari kufanya hivyo.

"Kama kunahitajika mtu afe ili Simba ichukue ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika, mimi nipo tayari kufanya hivyo," alisema na kutania "halafu nikifikia huko naenda kufungua tawi akhera".

Kaduguda alisema Simba ni kawaida yake kufanya vizuri katika michuano hiyo na kwamba mwaka 1993, walifika fainali kabla ya kufungwa na Stella Abidjan ya Ivory Coast, hivyo wanapaswa kuvunja rekodi hiyo kwa kutwaa ubingwa huo msimu huu.

Alisema kuna watu wanaumia na kuwabeza kutokana na mafanikio yao hayo kwenye michuano ya kimataifa, lakini imekuwa vigumu kwao kuweza kuwafikia.

Alisema mara ya mwisho kwa watani zao, Yanga kufika robo fainali ya Kombe la Shirikisho ilikuwa mwaka 1970 walipocheza na Asante Kotoko ya Ghana, hivyo wana wivu na mafanikio yao.

"Safari hii tumejipanga kuchukua ubingwa kwa sababu tuliwahi kufika hadi fainali ya michuano hiyo 1993, sasa hivi tunahitaji kuvunja rekodi yetu, tusiwape masikio watu ambao kila kukicha wanatubeza kwamba hatuna timu ilhali wanaona wivu mafanikio ya Simba.

"Wao kuingia hatua ya robo fainali ilikuwa ni mwaka 1970, lazima watu waumie, wanune ila tusijali maneno yao na twende tukajaze uwanja, kwa maandalizi yetu nina imani Orlando Pirates hachomoki kw Mkapa," alisema Kaduguda ambaye aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa klabu hiyo na kuongeza;

"Tunatakiwa kubadilika kutoka mfumo wa zamani wa kujinasibu kuchukua ubingwa wa nyumbani mara 27, huku kimataifa ikiwa ni aibu, Simba tumetoka huko tunataka kucheza fainali ya Afrika, maana tumechagua njia yetu ya kusonga mbele."

Naye Mwenyekiti wa klabu hiyo, Murtaza Mangungu alisema kuna watu macho yao yamejaa ukungu kwa kutoona jitihada za Simba kufikia mafanikio haya ya kutumikia nchini mzima.

Alisema Simba imefanikiwa kuingiza timu nne kwenda kucheza kimataifa kwa misimu mitatu, jambia ambalo linafanya kuonekana soka la Tanzania limepanda.

"CAF wanaizungumzia Simba ni klabu bora, utashangaa anatokea mtu anasema kwamba si bora wakati kwa miaka mitatu inazipeleka timu nne za Tanzania kwenda kucheza michuano ya kimataifa," alisema Mangungu na kuwataka mashabiki wa Simba kutowapa nafasi hao ambao wamekuwa wakiibeza timu yao na badala yake wajitokeza kwa wingi uwanjani Jumapili kushuhudia timu hiyo inavyopata ushindi mnono dhidi ya Orlando Pirates.

Alisema: "Hatuwabezi Orlando Pirates, tunawaheshimu kwa sababu ni timu ambayo iliwahi kuchukuwa ubingwa wa michuano hii, niwahakikishie timu yetu iko vizuri na inaendelea na maandalizi ya mchezo huo wa Jumapili".

Alisema milango ya uwanjani Jumapili itafunguliwa kuanzia saa 9:00 mchana badala ya mapema zaidi kama ilivyozoeleka, hiyo ikiwa ni kutokana na kuwapo kwa mashindano ya kusoma Quran siku hiyo. Kwa upande wa Mwenyekiti wa Wazee wa Simba, Hassan Dalali, aliomba viongozi kupatiwa siku moja kabla ya mchezo kwenda kambini kuzungumza na wachezaji wao.

TUUJAZE UWANJA...



Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu, akizungumza na mashabiki wa timu hiyo wakati wa uzinduzi wa kampeni ya hamasa kuelekea mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates itakayopigwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa. Uzinduzi huo ulifanyika Chang'ombe Maduka Mawili wilayani Temeke, Dar es Salaam jana. Kulia ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Mwina Kaduguda. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yaanza maandalizi 'dabi'

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wa Yanga wanarejea leo mazoezini kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya 'dabi' ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya watani zao wa jadi, Simba, inayotarajiwa kuchezwa Aprili 30, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, amesema baada ya mechi ya Kombe la FA dhidi ya Geita Gold FC na kufanikiwa kuingia hatua ya nusu fainali, wachezaji walipewa mapumziko ya siku mbili na sasa wanaanza mazoezi rasmi 'kumuwinda 'Mnyama'.

"Mazoezi yataanza kesho Jumatano (leo), na ni maandalizi sasa ya mechi ya 'dabi', kwani tutakaa na mwalimu Nasreddine Nabi atuambie anahitaji nini kwa ajili ya kukamilisha mipango ya mechi hiyo ambayo tunatarajia itakuwa ngumu na utakuwa nzuri, kwa hiyo sasa akili yetu tunaelekeza kwenye mechi hiyo," alisema Bumbuli.

Alisema lengo lao si tu kuifunga Simba kutokana na utani wa jadi uliopo baina yao, lakini ni kutaka kutanua pengo la pointi lililopo, ili wawe kwenye mazingira salama ya kuutwaa ubingwa msimu huu.

"Tunajiandaa kuongeza wigo wa pointi, kutoka 10 mpaka kufikia 13, wapo wengine tumewazidi mpaka pointi 20, lakini kuna hii timu inatusogelea sana, tunataka tuwe naye mbali kwa pointi 13, hilo ndilo lengo letu," alisema Bumbuli.

Yanga kwa sasa ndiyo vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa imekusanya pointi 51, na ndiyo timu pekee ambayo mpaka sasa haijapoteza mechi yoyote kwenye ligi, ikicheza mechi 19, ikishinda 16 na sare tatu, ikifuatiwa na Simba yenye pointi 41, na Azam FC inashika nafasi ya tatu kwa pointi zake 28.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042